BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,016,428,582/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**ACT**- Wazalendo yashauri TICTS isiongezewe mkataba




UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Julai 22, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581014

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

## HOMA YA MGUNDA:
# Tahadhari yatolewa walaji nyama choma

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza katika Mkutano wa 22 wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), jijini Arusha jana. Kulia ni Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta. **PICHA: IKULU**

# Mambo 5 mkutano wakuu EAC

UKURASA 3



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbalawa (kulia), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alipowasili katika ufunguzi wa kongamano la uwezeshaji kwa makandarasi na wazabuni nchini, lililoandaliwa na Benki ya CRDB, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki hiyo, Boma Raballa, Mkurugenzi wa Mawasiliano, Tully Mwambapa na Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Benki hiyo, Toyi Ruvumbangu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# IGP mpya atangaza kuanza kazi na wahalifu

UKURASA 2

**MICHEZO** MANARA NJIA PANDA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

# ...Wataalamu wataja mbinu kuukabili mgunda nyumbani

**Na Jenifer Gilla**

WATAALAMU wa magonjwa na mifugo nchini wametoa mbinu mbalimbali za kujikinga na ugonjwa wa mgunda majumbani baada ya kuthibitisha kuwapo kwa watu wanaougua ugonjwa huo nchini.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Hezron Nonga, alisema jana kuwa ili kujiepusha na maambukizi ya ugonjwa huo jamii ihakikishe nyama wanazokula, zimepimwa na wataalamu na kuthibitishwa usalama wake na kuwa makini na nyama za porini, hasa panya.

"Tunawashauri watu kwamba waache kula vitu visivyoliwa kikawaida, wale panya ndiyo chanzo cha shida na kule Mtwara na Lindi wanawala sana wale panya," Prof. Hezron alionya.

Kuhusu mifugo, Prof. Hezron alisisitiza jamii ihakikishe inawapatia chanjo na kupunguza mwingiliano wa wanyama wa kufugwa na wa porini ili kuepusha maambukizi kwa kuwa binadamu wapo karibu na wanyama hao.

"Kwa maana hiyo ni kwamba kwa sababu mbwa anafugwa katika mazingira ya nyumbani, watu wachukue tahadhari ya kudhibiti panya, kwa sababu ndiyo chanzo kikuu cha ugonjwa huu kuja kwenye mazingira ya nyumbani.

"Hawa ndio wanautoa kwa wanyama wa porini huko kama simba, nyati na kuuleta huku," alifafanua.

Alisema utafiti unaonyesha kuwa ipo mifugo na wanyama wengi wa porini ambao wana maambukizi lakini hawaugui huku wanyama kama ng'ombe, kiwango cha maambukizi kikiwa ni asilimia 5.5 mpaka 50 kulingana na eneo.

Mkurugenzi wa Kuratibu na Kukuza Utafiti wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Dk. Paul Kazyoba, akizungumza na RadioOne jana, aliishauri jamii isipende kwenda kulisha mifugo kwenye mazingira yenye wanyamapori kwa kuwa huko ndiko wanaambukizwa magonjwa hayo.

Pia alishauri mifugo ichinjwe kwenye maeneo rasmi ili nyama yake ikaguliwe na wataalamu wa afya kama ni salama kwa matumizi ya binadamu, pia kula nyama iliyoiva vizuri na maziwa au maji yaliyochemshwa vyema.

Mkurugenzi huyo aliitaka jamii kuzingatia usafi wa mazingira ya nyumbani ili kudhibiti wanyama hasa panya ambao kuingia kwao ndani kunawaachia bakteria wanaosababisha ugonjwa huo.

Mkurugenzi wa NIMR, Sayoki Mfinanga, aliishauri jamii inayofuga, ihakikishe inapeleka mifugo hiyo kwa wataalamu wake pale wanapoona wanaugua ili kufanyiwa vipimo, kupatiwa dawa na ushauri.

Mwanzoni mwa wiki, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema ugonjwa huo ni miongoni mwa magonjwa yanayoambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu na unasababishwa na bakteria aina ya leptospira interrogans.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Balozi wa China hapa nchini, Chen Mingjian, kabla ya mazungumzo yao, ofisini kwake, Ikulu Magogoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

# Tahadhari yatolewa walaji nyama choma homa mgunda

**Na Martha Magawa**

SERIKALI kupitia Wizara ya Afya imewataka wananchi kuchukua tahadhari wanapohitaji kula nyama choma kwa kuhakikisha chanzo chake ni salama na inaiva vizuri ili kuepukana madhara kwa walaji.

Rai hiyo ilitolewa na Dk. Azma Simba, kutoka wizara hiyo ambaye ni mtaalamu wa afya ya jamii katika fani ya epidemiolojia wakati akizungumza na Nipashe kupitia mahojiano.

Azma alisema kuwa ulaji wa nyama ambayo haijaiva vizuri ni hatari kwa afya ya walaji na kuwataka wananchi wachukue tahadhari wakati tayari serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi wa mikoa ya Kusini mwa Tanzania kulikotangazwa mlipuko wa ugonjwa wa Mgunda na kuripotiwa watu 20 kugundulika kuwa nao na watatu kati yao kupoteza maisha.

"Kwa wale watumiaji wa mishikaki au nyama choma yoyote wahakikishe kuwa vyanzo vyao ni salama na nyama ile inakuwa imekaguliwa ili kuepusha madhara ya kiafya ikiwamo homa ya Mgunda na magonjwa yoyote yanayoambukizwa na wanyama," alisema Azma.

Pia, alisema Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wizara nyingine ikiwamo Maji, wataalamu wa mazingira na wanyama pori, wafanyakazi kwa pamoja chini ya mpango wa Afya Moja 'One Health' utasaidia kuondoa au kumaliza adha wanazokutana nazo wafugaji ikiwamo ukosefu wa majisafi na salama kwa jamii za wafugaji.

"Milipuko ya magonjwa yatokanayo na mifugo chanzo kikubwa ni kukosekana kwa huduma za majisafi na salama kwani wafugaji wanatumia maji pamoja na wanyama na mara nyingi bila kuchemsha maji hayo," alisisitiza Azma.

Wakati huo huo, Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania, Dk. Shadrack Mwaibambe, alisema ongezeko la wafugaji katika mikoa ya Kusini limetokana na wafugaji wengi kuhamia kutoka mikoa ya Kanda ya Kati na vyanzo vya maji kuzidiwa.

Kuhusu masuala yanayohusu afya, alisema wamekuwa wakiachiwa mzigo kubwa wataalamu wa afya jambo ambalo amelitaja kuwa sio sahihi na kushauri wanasiasa kuongeza nguvu kwa kuzungumza na wananchi wao ili kwa pamoja elimu iwafikie kwa wingi ili kuepusha athari zinazotokana na magonjwa ya milipuko.

# IGP Wambura aanza na wahalifu

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi, IGP Camillus Wambura, ametangaza vita dhidi ya wahalifu, akionya kuwa kamwe wasifikiri ni ajira kwa kuwa jeshi litatumia nguvu kubwa na za kisasa kuhakikisha wananchi wanakuwa salama na serikali inaendelea na shughuli zake.

IGP Wambura alitoa kauli hiyo kwa nyakati tofauti juzi baada ya kuapishwa kushika wadhifa huo na jana asubuhi alipoanza kazi rasmi na kuonekana akiwa jijini Arusha kwa ajili ya Mkutano wa 22 wa Wakuu wa Nchi saba za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Juzi baada ya kuapishwa, aliripoti Makao Makuu ya Polisi jijini Dodoma na kukabidhiwa rasmi ofisi na mtangulizi wake, Simon Sirro, ambaye ameteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania huko Zimbabwe.

Akizungumzia mikakati yake ndani ya Jeshi la Polisi, IGP Wambura aliitaja mitatu, ukiwamo wa kukabiliana na uhalifu nchini.

"Mikakati yangu mikubwa ambayo nitatekeleza kwa kushirikiana na makamishna walio chini yangu pamoja na kada mbalimbali za askari na viongozi waliopo ndani ya Jeshi la Polisi, kwanza ni kuhakikisha suala la uhalifu mapambano dhidi ya uhalifu yanaimarishwa.

"Wahalifu wasije wakafiriki kwamba ile ni ajira, hakuna hiyo na nguvu ambayo tutatumia kupambana na uhalifu ni kubwa lakini nguvu ya kisasa.

"Na tutahakikisha wananchi wanakuwa salama na serikali inaendelea na shughuli zake na kutokuwa na fikra za kuona ni namna gani wataanza tena kushughulika na uhalifu na kuweka rasilimali zao pale. Kazi yangu kubwa ni kuhakikisha suala la uhalifu linakoma," alionya.

IGP Wambura alitaja jambo la pili ni kushughulika na maadili ndani ya Jeshi la Polisi, akisisitiza hawawezi kuwa na jeshi zuri, imara la kisasa na lenye weledi kama hakuna maadili na nidhamu.

Alitaja suala la tatu ni haki kwa wananchi, akifafanua kuwa linajumuisha kuwa na vituo vya polisi vingi na kuhakikisha kuna askari wanaofanya kazi.

"Tunataka kuona watu wanatendewa haki kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa taratibu. Hii ni baadhi ya mikakati ambayo nitahakikisha inafanyiwa utekelezaji, inakuwa inasimamiwa na yote itaweza kuleta tija katika Jeshi la Polisi," alisema.

Akiwa jijini Arusha jana, IGP Wambura alisema Jeshi la Polisi limejipanga kuhakikisha wakati wote wa mkutano huo, kunakuwa na ulinzi madhubuti kwenye maeneo yote.

Juzi, Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kumwapisha IGP Wambura, alisema anachotegemea kutoka kwake ni mabadiliko makubwa ndani ya Jeshi la Polisi ili kuwe na ufanisi ndani ya jeshi hilo, pia usalama wa raia na mali zao uimarishwe.

# Makosa ubakaji kukosa dhamana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKOSA ya ubakaji na ulawiti yapo mbioni kuondolewa dhamana kutokana na serikali kuanza mchakato wa kufanyia marekebisho Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Hatua hiyo imetokana na utafiti mdogo uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuonesha kuwa baadhi ya watuhumiwa wa makosa hayo wakiwa nje kwa dhamana wanakimbia na wengine kuharibu ushahidi au kumalizana na wazazi ama ndugu wa muathirika wa vitendo hivyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Happy Msimbe, aliyasema hayo jana kwenye kikao kilichowakutanisha wataalam na wadau wa masuala ya sheria kutoka Wizara, Taasisi za serikali ili kutoa mapendekezo ya sheria hiyo.

Alisema nia ya kukutana na wataalam hao ni kupata maoni yatayosaidia kujenga hoja ya kufanya makosa hayo kutokuwa na dhamana ili kupunguza matukio hayo kwa jamii.

Mkurugenzi huyo alisema wanalenga kulinda kundi la watoto na wanawake ambao ni waathirika wa vitendo vya ukatili.

"Kikao hiki kimelenga kuangalia na kupitia sheria nyingine ambazo zinamgusa mtoto ili ziweze kuendana na hali halisi iliyopo katika jamii ili kuwasaidia watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili katika jamii," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ignas Mwinuka, alisema wameangalia pia katika sheria mbalimbali zikiwamo Sheria za Zanzibar ambazo zimeweka kosa la ulawiti kutokuwa na dhamana, ili kusaidia kuwalinda watoto na wanawake dhidi ya vitendo hivyo.

"Tumeangalia baadhi ya makosa hasa kosa la ulawiti hata ukilizingumza kwa jamii itakwambia kuwa ni sahihi kukosa dhamana hasa katika kulinda mila na desturi zetu," alisema Mwinuka.

Katika kikao hicho, wataalam hao walijadiliana namna bora ya kuhakikisha jamii inapata elimu ya kupambana na vitendo vya ukatili.

Kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi, Tanzania katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2021, matukio ya ukatili kwa watoto yaliyoripotiwa ni 11,499, huku makosa yaliyoongoza kwa idadi kubwa ni ubakaji (5,899), mimba kwa wanafunzi (1,677) na ulawiti (1,114).

Mikoa iliyoongoza kwa matukio ya ukatili ni Arusha (808), Tanga (691), Shinyanga (505), Mwanza (500) na mkoa wa kipolisi Ilala (489).

# Mambo matano aliyosema Rais Samia mkutano wa wakuu EAC

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amezungumza mambo matano ili nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zipige hatua kiuchumi ikiwamo kujikita katika kilimo cha umwagiliaji badala ya kutegemea mvua.

Akizungumza jana katika mkutano wa 22 wa Wakuu wa Nchi za EAC mjini hapa, Rais Samia alisema kilimo cha umwagiliaji ndiyo njia pekee itakayoziwezesha nchi za jumuiya hiyo kuwa na uhakika wa chakula.

Kwa mujibu wa Rais Samia, dunia hivi sasa inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi, hivyo kuna umuhimu wa nchi hizo kufanya kilimo cha umwagiliaji badala ya kutegemea mvua ambazo hazina uhakika.

Pia alitoa rai kwa nchi hizo kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara na reli ili mazao yanapotoka shambani yafike sokoni kwa urahisi.

"Tunatakiwa kuendelea kuwa na miundombinu bora na imara ambayo itakuwa chachu ya ukuaji wa uchumi kwa kuwa mazao yakitoka shambani moja kwa moja yatakwenda sokoni kwa haraka zaidi," alisema na kuongeza kuwa kuna umuhimu kwa nchi za EAC kulipa kipaumbele suala la usalama wa chakula.

Alisema kuna umuhimu kwa nchi za EAC kuzalisha kwa wingi ili kuwa na chakula cha kutosha na kuzisaidia nchi zingine zenye uhitaji kwa kuwa kuna maeneo ya kutosha ya kilimo.

Sambamba na hilo, alisisitiza umuhimu wa kuweka akiba ya kutosha ya mbegu kwa kuzihifadhi kwenye vihenge ili ziwe kwenye usalama ambao utaleta matokeo chanya hasa kwa maeneo ya vijijini.

Naye Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, alisema ili nchi hizo zifikie malengo, zinatakiwa kuimarisha miundombinu hasa barabara pamoja na kuweka kipaumbele katika suala la viwanda ili kukuza uchumi.

"Kuwapo kwa miundombinu imara na rafiki kutasaidia kusafirisha malighafi kutoka nchi moja kwenda nyingine na kufika sokoni," alisema Kenyatta.

Pia alisema kuwapo kwa soko huru la bidhaa la Afrika Mashariki, kutawaunganisha wanachama kiuchumi na kibiashara.

"Tukiimarisha soko huru na la pamoja itatusaidia kuuza mazao yetu kwenye masoko na kupunguza umaskini kwa wananchi wetu. Ifike wakati nchi za EAC tufikie hatua ya kujitegemea kiuchumi na kibiashara kwa kuwa na miundombinu imara ya reli na barabara,"alisema.

Kenyatta pia aliwaonya mabeberu kuingilia nchi za Afrika kwenye masuala mbalimbali yanayohusu mataifa hayo.

"Mfano kwenye suala la madini, wanapenda kutulaumu kuwa tunawatumikisha watoto wadogo kwenye uchimbaji lakini hakuna hata siku moja wameyakataa ila wanakuja kutugawanya na kutuuzia rasilimali zetu," alisema.

Viongozi wengine walioshiriki mkutano huo ni Rais Yoweri Museveni wa Uganda ambaye ni Mwenyekiti wa EAC na Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye. Marais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Rwanda na Sudan Kusini waliwakilishwa na viongozi wengine.

**Imeandikwa na Allan Isack na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA.**



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga (mwenye koti jeusi), akishuhudia kampeni ya uhamasishaji na utoaji wa chanjo ya UVIKO-19, mjini Iringa, jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# ACT-Wazalendo yashauri TICTS isiongezewe mkataba

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimeishauri serikali kusitisha kuongeza mkataba na Kampuni Binafsi ya Kimataifa ya Kuhudumia Makontena (TICTS), kwa madai imeshindwa kukidhi matarajio.

Kadhalika, imetoa mapendekezo matano kwa serikali ili kuboresha utendajikazi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), hasa kwenye ucheleweshaji wa mizigo na meli kuchukua muda mrefu huku nchi ikikosa mapato.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Msemaji wa Sekta ya Mawasiliano, Teknolojia, Habari na Uchukuzi wa ACT-Wazalendo, Ally Saleh, alisema kwa miaka mingi kumekuwa na mjadala wa mara kwa mara kuhusu utendaji kazi usioridhisha wa TICTS.

Alisema sehemu kubwa ya mjadala unawahusisha wadau wa biashara, viongozi, wabunge na wataalamu.

Alisema la pili ni kuunga mkono wadau wengine kuwa suala la ukodishaji au kutokodishwa tena TICTS lichukuliwe na lifanyiwe maamuzi katika hali ya uzalendo kwa maana ya kujali maslahi ya taifa. "La tatu serikali ifanye uchambuzi wa kina katika kutoa zabuni kwa kampuni zenye sifa ya kimataifa kwa kuipima TICTS kwenye utendaji wake mzima wa miaka 20 na faida zake na uwezo wa kufikisha malengo mapya yatakayokuwa katika mkataba ujao," alibainisha Saleh.

Alishauri pia serikali iwezeshe TPA kusimamia kitengo cha makasha cha Bandari ya Dar es Salaam, wakati wa mpito wakati ikiwa katika mchakato wa kutafuta mwekezaji mwingine.

Kadhalika, alidai kuwa imetajwa kwamba moja ya kilichochangia hali ya sasa ni serikali kutowekeza ipasavyo kwa yale inayowajibika nayo, na kushauri ni vyema jambo hilo lisimamiwe kwa umuhimu mkubwa ili kuongeza ufanisi.

Alisema matarajio ya kukodisha kitengo cha makasha katika Bandari ya Dar es Salaam yalikuwa ni kuboresha utendaji na kuongeza mchango wa sekta ya bandari katika uchumi wa taifa.

"Matarajio mengine ni kupunguza gharama za kuhudumia shehena za makasha zinazopita bandari yetu, ili kuhimili ushindani na nchi jirani, kuvutia shehena za ndani na nje na kuingiza teknolojia mpya na kuwawezesha wazawa kupata mbinu mpya za usimamizi na uongozi wa bandari," alisema Saleh.

Alibainisha kuwapo hoja kwamba taasisi hiyo haikufanikiwa kufanya yaliyotarajiwa kwenye matakwa ya mkataba na kwamba malalamiko ya utendaji wake yametiliwa mkazo na wafanyabiashara na waagizaji ambao wamekuwa wakibeba mzigo wa gharama za uchelewaji wa kufunga meli na kuondosha mizigo yao.

Alisema wakosoaji wa TICTS wanadai kwamba kwa mujibu wa mkataba taasisi hiyo ilitakiwa iwe inawekeza kuimarisha eneo la kuweka na kupokea makontena, akieleza kuwa katika mkataba wake ilitakiwa iwe inakuza huduma zake za kuhudumia makontena kwa asilimia 37 kwa mwaka jambo ambalo halikufanikishwa.

Vile vile, kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 2020/21 (CAG), ucheleweshaji wa ushushaji wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam, unasababisha malalamiko ya wateja na kuathiri ufanisi wa utendaji wa bandari.

"CAG alionyesha meli za mizigo na mafuta zinachukua wastani wa siku tatu hadi nane kupakua mizigo kinyume na mipango ya mamlaka ya bandari ya kuhakikisha inapunguza hadi kufikia siku mbili," alisema na kuongeza;

"Ni wazi kuwa kukaa kwa meli muda mrefu bandarini kunaathiri ufanisi wa mamlaka na kunapunguza ushindani wa kibiashara na bandari za nchi nyingine," alisema Saleh.




Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (wa nne kushoto), na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, wakizindua jarida la habari za Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA), katika mkutano mkuu wa 2022 wa chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Rais wa chama hicho, Godvictor Lyimo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Prof. Janabi: Unywaji sahihi pombe ni bia moja kwa saa

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete(JKCI), Prof. Mohammed Janabi, amesema unywaji sahihi wa pombe unatakiwa uwe chupa moja kwa saa.

Prof. Janabi alitoa kauli hiyo jana wakati akihojiwa na Kituo cha Televisheni cha Clouds, akishauri pia Watanzania kuzingatia muda sahihi wa chakula kwa ajili ya kulinda afya zao.

"Sijawahi kukataza chakula cha aina yoyote. Mimi ninachozungumzia ni aina gani ya chakula unachokula. Hili ni jambo kubwa sana. Kunywa pombe kwa wastani, tunakumbusha tena, chupa moja kwa saa, yaani kutoka chupa moja mpaka nyingine.

"Kwa hiyo, ukienda sehemu yoyote ya kunywa majira ya saa moja usiku, hakikisha mpaka saa mbili unakunywa chupa yako ya kwanza na saa mbili mpaka saa tatu unachukua chupa yako ya pili. Ule muda uliobakia tazama mpira, tamthilia na ukitoka hapo kapumzike.

"Jaribu pia kula mapema. Juzi nilikuwa natazama harusi ya wadogo zetu, nikaona chakula 'kimeseviwa' karibu saa sita (usiku) pale. Nikiangalia mpaka natetemeka. Nilikuwa nikamtania mke wangu, nikasema 'hawa wananihakikishia kazi yangu itakuwapo kwa muda mrefu kweli'.

"Bahati nzuri pale watu walikuwa wanacheza, lakini tuchukulie uko nyumbani, umekula saa nne, tano au saa sita usiku, ukitoka kwenye meza unakwenda kukaa kwenye kiti unachati kidogo na baada ya hapo unakwenda kulala.

"Kwa hiyo, msago wa chakula unaenda taratibu zaidi na kile kinachosagwa kinaenda kukaa stoo kwa sababu hakina matumizi," alifafanua.

Akizungumzia baadhi ya wagonjwa ambao hukimbilia kwenye mitandao ya kijamii kuomba barua baada ya kupewa vibali kwa ajili ya kwenda kuomba barua serikali za mitaa ili waingizwe kwenye matibabu ya msamaha, Prof. Janabi alisema ni vyema wanapojitokeza watu kama hao kuomba, taasisi hiyo ishirikishwe ili kuwasaidia zaidi.

"Kuna njia tatu au nne za malipo kwa ajili ya matibabu pale kwetu. Kuna wale wanaolipa kwa pesa taslimu, kuna asilimia kubwa inayolipa kupitia bima, kuna wale wanaochangia ambao kama operesheni ni Sh. milioni 10 na tukithibitisha kwamba hana uwezo wa kulipa hiyo pesa anatoa nusu halafu serikali inajazia iliyobaki.

"Na kuna wale ambao hawawezi kulipa kabisa. Hawa ndiyo imekuwa kidogo changamoto. Kiutaratibu ukija hata kama huwezi kulipia kabisa, upo utaratibu wa mtu kusamehewa. Tuna kitengo cha watu wa ustawi wa jamii ambacho huyu mgonjwa kama ni mzazi wa mtoto au ni mtu mzima ambaye hana uwezo, watakupa utaratibu baada ya kukuuliza maswali.

"Halafu watakuambia ukachukue barua kutoka kwa mwenyekiti wa serikali za mitaa inayosema kwamba huyu mama au huyu mzee hana uwezo na hana kazi.

"Na ikishathibitishwa pale inakwenda kwa mkurugenzi, wanaitwa Clinical Support Services, wanaoshughulikia hao. Yule naye akiithibitisha ndipo inakuja kwangu kama Mtendaji Mkuu na mimi ninaandika huyu aruhusiwe," alifafanua.

Alisema ni vyema kuendelea kukumbusha jamii juu ya matumizi ya msamaha huo.

"Ni kitu muhimu sana kukumbushia tena jamii kwamba upasuaji wa moyo ni tofauti na upasuaji mwingine unaofanywa na hospitali nyingine. Na utofauti ni kwamba, ukitaka kufanya operesheni ya apendex, unahitaji kisu na nyuzi na kile kisu unaweza kukisafisha na ukarudia tena tofauti na ilivyo kwa moyo.

"Sasa bahati mbaya inayotokea kwenye jamii, kwa mfano akipewa mama kwamba anatakiwa akachukue kibali kwenye serikali za mitaa, badala ya kwenda kule anakwenda kwenye mitandao ya kijamii au kwenye makundi ya WhatsApp kuomba msaada, kwamba amekataliwa.

"Kufanya hivyo kuna hatari mbili, moja watu wakiona hali ya mtoto wanaanza kuchangia. Na kama hamkuangalia huo mchango unaweza kwenda kwa muda mrefu zaidi na operesheni ikachelewa, lakini mtu anaweza kuchangiwa na akapata shida nyingine na kuitumia hiyo fedha. Kwa hiyo, ni vyema mtu kama huyu anapokuja kwenye jamii kuomba, tushirikishwe," alisema.

Alibainisha kuwa kwa mwezi wanasamehe kati ya Sh. milioni 100 mpaka 120 na kwamba katika mwaka wa fedha uliopita, walisamehe Sh. bilioni 1.4.

"Kwa hiyo tunaposema tunasamehe, wanatakiwa kujua kwamba kuna mtu anatakiwa kulipa.

Na ndiyo maana huwa tunafanya kampeni za kukusanya hizo fedha, kwa hiyo ni lazima tuwe waangalifu, hizi fedha tunazitumia namna gani kwa wale watu wanaohusika kabisa," alisema Prof. Janabi.

# Mambo yaiva ujenzi mwendokasi Tabata

**Na Martha Magawa**

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) umesema kuwa tayari rasimu ya taarifa ya wakazi wa Tabata Segerea jijini Dar es Salaam wanaotakiwa kupisha ujenzi wa barabara ya mwendokasi iko tayari na itakabidhiwa kwao Julai 29, 2022.

Meneja wa TANROADS mkoani humo, Harun Senkuku, ameliambia Nipashe kuwa mradi wa ujenzi wa barabara ya mwendokasi katika awamu ya tano kwa wakazi wa Segerea tayari mchakato uko mwishoni na timu ya uhamasishaji na tathmini ya mali imeshaanza kazi.

Senkuku alisema kuwa TANROADS inasubiri kupokea ripoti hiyo kwa awamu ya kwanza ili kufahamu ni wakazi wangapi watakwenda kupisha ujenzi huo na jumla ya fidia itakuwa kiasi gani kwa wananchi wote.

"Awamu ya kwanza ilikuwa ni uhamasishaji wa wananchi kukubali kupisha katika maeneo yao, tayari zoezi hilo limekamilika, hatua iliyopo ni tathmini ya awamu ya kwanza ya idadi ya familia zitakazopisha na jumla ya mali na hatua ya mwisho itakuwa ni sisi kujiridhisha uhalali wa thamani na mali zitakazolipwa kwa wananchi," alisema Senkuku.

Alisema malipo ya fidia yatafanyika kwa wamiliki halali na baada ya tathmini watapigwa picha wakiwa katika maeneo yao ili kuepusha mkanganyiko baadaye ambayo imekuwa ikijitokeza wananchi wanapokuwa wakilipwa fidia.

Alisema mpaka sasa bado kiasi cha fedha kitakacho gharimu mradi huo hakijajulikana mpaka pale watakapopata idadi ya nyumba na mabanda ya biashara.

Nipashe pia ilimtafuta Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Segerea, Samuel Binagi, ambaye amesema kuwa tayari wananchi wamekubaliana na hakuna waliopingana na zoezi hilo wote wanasubiria kutajiwa kiasi cha fidia zao.

"Mpaka sasa hakuna mgomo wowote kutoka kwa wananchi wangu, masuala ya uhamasishaji yamekamilika migogoro hutokea pindi malipo yanapokuwa tofauti, lakini mpaka sasa hakuna changamoto yoyote tunawasubiria TANROADS tu", alisema Binagi.

# Ubalozi watoa tahadhari wizi wa mtandao China

**Na Waandishi Wetu**

UBALOZI wa Tanzania huko China umetoa hadhari kwa Watanzania wanaopanga kununua bidhaa kwa kampuni zilizoko katika nchi hiyo kupitia mtandaoni kuwa makini ili kuepuka kuibiwa.

Taarifa iliyotolewa na Balozi wa Tanzania huko China, Mbelwa Kairuki, Watanzania wanakumbushwa kufanya upekuzi wa kampuni hizo kabla ya kufanya ununuzi na kuwa ubalozi huo unatoa huduma ya kuzitambua kampuni hizo. "Unapoanza mawasiliano na kampuni husika kwa ajili ya kununua bidhaa, omba upatiwe taarifa zifuatazo; jina la kampuni, anwani ilipo kampuni na namba ya simu.

"Vilevile, ofisa biashara unayewasiliana naye katika Kampuni hiyo akupatie nakala ya kitambulisho chake; na WECHAT ID," alisema balozi huyo.

Aliongeza kuwa kwa wanaotaka kununua bidhaa kutoka kwa kampuni zilizoko katika mtandao wa Alibaba, wanaweza kutumia huduma ya kulipia ya Trade Assurance Service inayotolewa na mtandao huo kumhakikishia mteja anapata bidhaa aliyoagiza.

Katika hatua nyingine, Ubalozi wa China nchini umefungua utoaji wa visa za kuingia China kuanzia Julai 11 mwaka huu.

Ubalozi huo pia umefanya mabadiliko ya masharti ya utoaji visa za kuingia nchini humo kwa kuongeza cheti cha chanjo ya UVIKO-19. Moja ya masharti hayo ni mwombaji kutoa uthibitisho wa ukaaji wa Tanzania kwa ambao ni wageni na vingine vinavyoonyesha sehemu anakofanya kazi, mwajiri na anakoishi.

■**Imeandaliwa na Jenifer Gilla na Romana Mallya**

# Mwinyi ataka kamati maalum baraza vyama siasa Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema wakati umefika wa kuundwa Kamati Maalum ya Baraza la Vyama vya Siasa na kujadili masuala maalum yanayohusu Zanzibar.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati akizindua kikao cha dharura cha Baraza la Vyama vya Siasa Tanzania, hoteli ya Madinat Al Bahr, Mbweni Zanzibar.

Alisema kwa vile chombo hicho ni cha Muungano, bado yako mambo yanatofautiana kisheria baina ya pande mbili za Muungano akitolea mfano mfano Sheria ya Tume ya Uchaguzi ambapo kuna sheria mbili, ile ya Zanzibar na ya Muungano.

Kutokana na hali hiyo, alisema kuchanganywa kwa masuala hayo, kunasababisha baadhi ya mambo kutofanywa vizuri kutokana na changamoto hiyo ya kuwa na sheria tofauti.

Dk. Mwinyi alisema ni matumaini yake kwamba kamati hiyo ikifanya kazi vizuri kwa kuainisha changamoto zote zinazohusu Zanzibar, kikosi kazi kitapata taarifa maalum inayohusu Zanzibar ili kitakapotoa ushauri kwa serikali kisije kupoteza fursa ya kuyashughulikia mambo yanayohusu Zanzibar.

Pia alisema licha ya mafanikio yaliyopatikana tokea mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa urejee nchini mwaka 1992 pia, kumekuwa na changamoto kadhaa ambazo baraza hilo limeviweka vyama vya siasa pamoja mara kwa mara katika kuzijadili kero na kutafuta ufumbuzi.

Watanzania, alisema wana wajibu na haki ya kujipongeza kwa kutimiza miaka 30 tangu mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa urejee mwaka 1992 na bado unaendelea kuimarika kwa amani, utulivu na umoja wa kitaifa.

Pia, Dk. Mwinyi alieleza wajibu wa Baraza la Vyama vya Siasa kutekeleza masuala muhimu yakiwamo kuwa chombo kikubwa cha siasa kuhakikisha viongozi wakuu wa vyama vya siasa wanashiriki vikao vya baraza hilo, likutane mara kwa mara, kulinda tunu za taifa pamoja na kujadili na kukemea watu wanaofanya vitendo vinavyolenga kuvunja amani, utulivu na umoja wa nchini.

Rais Mwinyi alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi kubwa anazofanya za kukuza na kudumisha demokrasia ya vyama vingi vya siasa hapa nchini.

Alisema Rais Samia amekuwa akitumia njia mbali mbali ikiwemo kuleta maridhiano ya kisiasa ambapo Julai 15, mwaka huu, alikuwa Pemba ambako alifanya mazungumzo na viongozi wa vyama vya siasa wanaoishi huko.

Alisema hata yeye amekuwa akikutana na viongozi wa vyama vya siasa kwa nyakati tofauti na kubadilishana nao mawazo kuhusu kudumisha demokrasia, amani na umoja wa taifa.

"Mimi ni muumini mkubwa wa maridhiano ya kisiasa yenye lengo la kuleta umoja wa kitaifa, hivyo naviomba vyama vya kisiasa kutuunga mkono kwa kuonesha nia thabiti ya ushirikiano wa kujenga nchi yetu", alisema.




Wakazi wa Manispaa ya Iringa, wakitazama ajali ya gari la Halmashauri ya Manispaa hiyo, lililopinduka baada ya kugongana na gari jingine dogo, eneo la Iruwasa, juzi jioni, ambapo dereva wake alijeruhiwa. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Shaka atia neno bil. 6.4/- za Rais Samia elimu

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, amesema iwapo Sh. bilioni 6.4 zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya elimu ya juu zikitumiwa vizuri, kutakuwa na mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu.

Shaka aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipotembelea maonyesho ya 17 ya elimu ya juu huku akibainisha kuwa fedha hizo zinakwenda katika mradi maalum wa kuboreha elimu.

"Sh. bilioni 985 ambazo zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2022/23 zitakwenda kuboresha miundombinu ya vyuo vikuu na kuwapatia taaluma wahadhiri, kuweka majengo na vitendea kazi.

Tunaamini inakwenda kutoa fursa ya kuwaandaa vijana wengi kunufaika katika kada hiyo," alisema.

Shaka alisema changamoto kubwa waliyo nayo wakifuatilia taarifa ya chama cha waajiri Afrika Mashariki ni kwa wahitimu katika mazingira ya kujiajiri na kuajirika hairidhishi.

Alisema serikali imeliona jambo hilo, hivyo fedha hizo zilizotengwa zitakwenda moja kwa moja kwenye maarifa na kuwajengea ujuzi wahitimu ili wakimaliza waweze kuajirika.

Alisema CCM inaridhishwa na hatua zinazochukuliwa na serikali katika kuweka mazingira mazuri na rafiki huo ni uwezeshaji wa kiwango cha juu.

Shaka alisema hayo yote yanayofanywa ni utekelezaji wa ilani ya CCM ya 2020/25 ibara ya 80 na 102 zilizoeleza vizuri namna gani serikali zitakavyoweka mazingira rafiki, kujenga uwezeshaji mkubwa ili kuwekeza katika sekta ya elimu kwa kuamini kuwa sekta hiyo ndio iliyobeba uti wa mgongo kwa taifa.

Alisema awali alikuwa anapokea malalamiko mengi ofisini kwake kuhusiana na taasisi hiyo ya elimu na kwa sasa mambo yamebadilika.

Pia alisema wamefika kuona maonyesha hayo namna ambavyo serikali waliyoipa dhamana ya kutekeleza ilani ya chama inavyofanya yale waliyoahidi katika kipindi cha miaka mitano.

Alisema ameona namna maboresho makubwa yamefanywa katika sekta ya elimu kupitia vyuo vikuu mbalimbali vilivyoshiriki na amejionea utoaji wa huduma moja kwa moja ambao kwa kiasi kikubwa umeondoa urasimu kwa wahitaji.

"Maonyesho haya yanasaidia kuleta huduma hizi muhimu karibu na wanaohitaji kwa niaba ya chama ninawashukuru serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya elimu," alisema

"Ukitaka kuona mabadiliko makubwa yamefanyika kwa namna gani tulikotoka na tulipo na matarajio yetu tumeambiwa kuna ongezeko la wahitimu, ni hatua kubwa hii ni kwa sababu ya kuwepo kwa mazingira rafiki na Rais ndiye aliyetengeneza hayo mazingira," aliongeza.

Shaka alisema katika mwaka huu wa fedha Rais Samia ametengeneza mazingira rafiki kwa vijana ambao ni wanufaika wa elimu hasa katika taasisi hizo za elimu ya juu na wameongezewa bajeti.

Alisema Rais Samia ameonyea nia kwa kupunguza tozo kutoka asilimia sita hadi asilimia 10 kwa wanufaika wa elimu ya juu na kwamba Rais amesamehe Sh. trilioni 1.1 deni ambalo halilipiki kwa bodi ya mikopo hii ni hatua kubwa iliyofanywa.

Naye Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Prof. Charles Kihampa, alisema serikali imewapatia Sh bilioni 6.4 kwa muda wa miaka mitano na fedha za miezi sita ya kwanza wameshazipokea.

Alisema fedha hizo ni kwa ajili ya kulinganisha mifumo ya udhibiti wa ubora, mafunzo ya uongozi, mapitio ya mitaala ambayo imeshaanza na ipo timu ambayo inaendelea kupokea maoni.

## Mtuhumiwa mauaji watu wawili asakwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma limeanza msako wa muuaji wa watu wawili wanaodaiwa kuwa ni wapenzi waliouawa kikatili kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali katika eneo la Makulu, jijini Dodoma.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Martin Otieno, alisema watu hao waliuawa majira ya saa 11 alfajiri juzi na jeshi hilo linaendelea kumsaka aliyefanya tukio hilo.

Alisema inasemekana chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa mapenzi.

"Wameuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali kifuani na mwanamke upande wa titi la kushoto," alisema.

Aliwataja waliouawa kuwa ni Esther Shiyago (25) Mhitimu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), ambaye anadaiwa alikuwa miongoni mwa watu waliokuwa kwenye usaili wa makarani wa sensa na dereva wa bodaboda Dominic Kigula (31).

MAJIRANI WAFUNGUKA

Akizungumzia tukio hilo, jirani wa marehemu, mkazi wa Mtaa wa Msangalale-Makulu, Irene Shayo, alisema alisikia kelele alfajiri kwenye nyumba hiyo na akadhani ni ugomvi wa kawaida wa ndani, lakini asubuhi baada ya kupambazuka na kutoka nje alikuta damu zikiwa zimetapakaa kuanzia mlango wa kuingilia ndani huku miili ya watu ikiwa mmoja sakafuni na mwingine kitandani.

Naye Victoria Peter alisema akiwa chumbani kwake asubuhi alisikia sauti za vyombo vikigongana ndani ya chumba cha marehemu Dominic na sauti za chini chini, baada ya muda mfupi alisikia mtu akitoka.

"Nilipotoka nje nilikuta mlango wazi mwili wa mwanamke sakafuni utumbo ukiwa nje na mwanaume akiwa kitandani nikarudi ndani kwa haraka kwa uoga nikaanza kupiga simu...maana awali nilisikia mtu ndani anamwambia jamaa ngoja nikueleweze, lakini ghafla kukawa kimya," alisema.

Henry Masanja, anayefanya kazi ya bodaboda na marehemu Dominic, alisema; "kuna mtu anatajwa alikuwa kwenye mahusiano na huyu binti na alimsomesha na alimfungulia duka hapa hapa Makulu, lakini Esther alilifunga na kwenda kwao Tabora."

Alisema binti huyo alimaliza chuo mwaka jana akaenda kwao, lakini juzi alikuja hapa kutoka Tabora baada ya nafasi za wasimamizi wa sensa kutoka.

**NDUGU WA MAREHEMU**

Mdogo wa marehemu, Frank Kigula alisema, alikuwa anamfahamu mwanamke (marehemu) huyo kama mfanyabiashara wa duka sio mpenzi wa marehemu kaka yake, hakuwahi kumshirikisha chochote.

Alisema mazishi ya Dominic yatafanyika leo jijini hapo.

Mzazi mwenzie na marehemu Dominic, Judith Felix alisema, hajawahi kufahamu kama mwanaume wake alikuwa na mtu mwingine kimahusiano kwa kuwa hadi Jumapili (Julai 15, mwaka huu) asubuhi alitoka kwake akienda kazini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mchakato marekebisho Sheria Makosa Jinai ufanyike haraka

**TAARIFA** kuwa makosa ya ubakaji na ulawiti yapo mbioni kuondolewa dhamana zinatia moyo kutokana na vitendo hivyo kushamiri katika maeneo mbalimbali nchini.

Taarifa zinasema serikali inatarajia kuanza mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Suala la watu wanaotuhumiwa kufanya ukatili wa kijinsia ukiwamo ubakaji, udhalilishaji wa watoto, kuachiwa kwa dhamana wanapofikishwa mahakamani, limekuwa likilalamikiwa na watu wengi.

Malalamiko hayo yanatokana na baadhi ya washtakiwa hao au watuhumiwa wanapoachiwa hurudi mitaani na kuendeleza vitendo hivyo.

Utafiti mdogo uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka umegundua kuwa baadhi ya watuhumiwa wa makosa hayo wakiwa nje kwa dhamana wanakimbia na wengine kuharibu ushahidi au kumalizana na wazazi ama ndugu wa mwathirika wa vitendo hivyo.

Wanaharakati wa haki za binadamu na wadau wanaotetea haki hizo, kila mara wamekuwa wakiomba marekebisho ya sheria ili zile zenye upungufu ziweze kurekebishwa na kutenda haki.

Katika mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, serikali inakusudia kukutana na wataalamu kupata maoni yatakayosaidia kujenga hoja ya kufanya makosa hayo kutokuwa na dhamana ili kupunguza matukio hayo kwenye jamii.

Hatua hiyo ni ya kupongezwa kwa sababu kila siku kumekuwa na matukio ya udhalilishaji na ukiukwaji wa haki za binadamu kutokana na vitendo vya ukatili.

Serikali imesema katika marekebisho hayo wanalenga kulinda kundi la watoto na wanawake ambao ni waathirika wakubwa wa vitendo vya ukatili.

Pia imeelezwa kuwapo nia ya kupitia sheria nyingine ambazo zinamgusa mtoto ili ziweze kuendana na hali halisi iliyoko katika jamii kuwasaidia watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili katika jamii.

Wameangalia pia katika sheria mbalimbali zikiwamo sheria za Zanzibar ambazo zimeweka kosa la ulawiti kutokuwa na dhamana ili kusaidia kuwalinda watoto na wanawake dhidi ya vitendo hivyo.

Katika kuangalia suala hilo, baadhi ya makosa hasa ya ulawiti inaonyesha yakizungumzwa kwa jamii, itakwambia ni sahihi kukosa dhamana hasa katika kulinda mila na desturi za Tanzania.

Ni matumaini yetu kuwa wataalamu waliokutana kujadiliana namna bora ya kuhakikisha jamii inapata elimu ya kupambana na vitendo vya ukatili, watahakikisha mchakato huu unakwenda haraka ili watoto na wanawake wanaofanyiwa vitendo hivyo waweze kulindwa.

Kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2021, matukio ya ukatili kwa watoto yaliyoripotiwa ni 11,499, huku makosa yaliyoongoza kwa idadi kubwa ni ubakaji (5,899), mimba kwa wanafunzi (1,677) na ulawiti (1,114).

Mikoa iliyoongoza kwa matukio ya ukatili ni Arusha (808), Tanga (691), Shinyanga (505), Mwanza (500) na Mkoa wa Kipolisi Ilala (489).

Vitendo hivyo vya ukatili sasa hivi vimekuwa vikishuhudiwa kufanyiwa watoto wa kiume, tofauti na ilivyokuwa imezoeleka kuwa wanaofanyiwa ukatili huo ni wa kike.

Wazazi, walezi na jamii ni jukumu letu pia kutoa ushirikiano ili tatizo hili liweze kukomeshwa kabisa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Jamani ndugu Machinga Mwanza, hiari ni muhimu kuliko kutimuana

Na Anthony Gervas, Mwanza

**BAADHI** ya Machinga jijini Mwanza, wamekuwa hawataki kutii sheria bila ya shuruti, kurejea agizo la serikali la kuwaondoa katikati ya miji nchi nzima na kuwatengea maeneo rasmi ya kufanyia biashara zao.

Wapo ambao bado wanaendelea kukaidi marufuku ya serikali, kutofanya biashara katikati ya jiji, badala yake waende kwenye maeneo waliyotengewa.

Wafanyabiashara hawa wamekuwa wakirejea katikati ya jiji katika mitaa ya Soko kuu, Rwagasore pamoja na Makoroboi inapofika saa tisa alasri.

Hivi kumbe wamezoea kila wakati kusukumwa kwa nguvu na vya polisi au mgambo wa jiji. Niulize, kuna sababu gani za kuendelea kupambana na serikali, kukamatwa na kutaifishwa bidhaa au kutozwa faini na kupata hasara zaidi? Ni wazi hakuna hoja!

Mtu akipita katika mitaa niliyoitaja majira hayo, anakuta wameshaanza kupanga bidhaa zao mbalimbali pembezoni mwa barabara mbele ya maduka ya wafanyabiashara wakubwa, hata kusababisha kero kwa watembea kwa miguu wanaoegesha magari yao madogo.

Polisi na mgambo nao hawachoki kuhakikisha wanawakabili, kwa hatua kali za kisheria, ili kutimiza agizo la rais la wafanyabiashara wote wadogo kwenda kwenye maeneo rasmi waliotengewa.

Nimekuwa nikishuhudia wakikamatwa na wengine wakikimbia na bidhaa zao au kukimbia nazo kwenye mifuko, wanapostukizwa ghafla na polisi au mgambo wanapopita mtaani kuhakikisha maeneo yote yanabaki wazi.

> **Nimekuwa nikishuhudia wakikamatwa na wengine wakikimbia na bidhaa zao au kukimbia nazo kwenye mifuko, wanapostukizwa ghafla na polisi au mgambo wanapopita mtaani kuhakikisha maeneo yote yanabaki wazi.**

Lazima nikiri, kuondolewa wafanyabiashara hao katikati ya jiji, kuna faida zake ambazo zimesaidia kuondoa hali ya uchafuzi wa mazingira kama ilvyokuwa awali, ikiwamo mifereji ya maji kuziba na mitaro kujaa taka mbalimbali.

Hoja yao kuu Machinga ni kwamba, biashara kule waliko ni ngumu kutokana na maeneo mengi waliopelekwa kutokuwa yamekamilika kama vile stendi ndogo za daladala.

Waswahili hunena, mvumilivu hula mbivu, lakini hawa wanasema uvumilivu kwao ni mtihani, kutokana na kudai kukatika mitaji baadhi yao na kufunga biashara, wakijenga hoja kwamba 'hesabu za kujumlisha na kuzidisha' hakuna tena zilizopo ni 'za kutoa.'

Mimi naamini serikali inaendelea kufuatilia vilio vyao na kuchukua hatua mbalimbali, kupitia watendaji waliopewa dhamana ya kusimamia na kutatua changamoto hizo.

Tabia ya watendaji kubaki ofisini na kutojali shida za wananchi ni zama zilizopitwa na wakati. Nanyi msisubiri mpaka kunyooshewa vidole, ndio muanze kuchukua hatua kishingo upande mnawaumiza wananchi.

Kauli ya vijisenti bado inaendelea. Siku zote mwenye nguvu huitwa 'pawa' kumbe msamiati wa mbuzi hula kwa urefu wa kamba yake umesharudi kwa wananchi, je kamba ikiwa fupi na nyasi hazipo atakula mchanga?

Mkuu wetu Hangaya, hawa watendaji wanaosimamia miradi yetu, halafu haieleweki kukamilika, unawaonaje wanafaa au hawafai? Najua jibu lako ni hapana, tena kubwa...


Mbona visingizio haviishi? Kila siku vinaibuka na vipya, mara 'hoo' gari halikuwa na mafuta leo kwenda saiti, 'hoo' bajeti yetu haijakaa sawa, imebana tunasubiri ijayo, allah Uviko-19 nao umeingilia kati tungekuwa tumekamilisha miradi ya wananchi.

Mara utasikia toba na vita tena vya Ukraine na Russia vimeingia hadi kwetu kutuathiri hara kwa hili! Jamani ndugu zangu, tuwe wavumilivu, majibu hayo yanafurahisha au yanaudhi?

Nauliza mmesahau kwamba visingizio vya aina hiyo mlikuwanavyo tangu zamani za kale, kabla ya hivyo vya sasa, ipo miradi mingi ilishatelekezwa miaka mingi haina majibu ya msingi kwanini haijakamilika.

Nahitimisha nikisema. Watanzania tumeshachoka kudanganywa, lengo letu ni moja tu, maendeleo!

# Balozi China aona nuru ya maendeleo Afrika



Balozi wa China nchini Tanzania , Chen Mingjian

**BALOZI Chen Mingjian amefanya mahojiano kwa maandishi na waandishi wa vyombo vya habari vya ndani ikiwa ni baada ya kuwapo nchini miezi sita tangu alipowasili. Katika mahojiano hayo, anazungumzia mambo kadhaa kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na nchi za Afrika...**

**SWALI**: Ni maeneo gani China na Afrika zimefanya ushirikiano kwa vitendo?

**BALOZI CHEN:** Tangu kuwasili kwangu zaidi ya miezi sita iliyopita, kupitia mazungumzo yangu na Rais Samia Suluhu Hassan na watu katika nyanja mbalimbali, ninaweza kuhisi shauku ya Tanzania kupata maendeleo huru.

Mkutano wa Nane wa Mawaziri wa FOCAC ulifanyika kwa mafanikio Novemba, mwaka jana. Katika sherehe za ufunguzi, Rais Xi Jinping wa China alitangaza kuwa China na nchi za Afrika zimeandaa Dira ya China na Afrika 2035.

Chini ya mpango wa kwanza wa miaka mitatu wa dira hiyo, China itafanya kazi kwa karibu na nchi za Afrika kutekeleza programu tisa zikiwamo matibabu na afya, mpango wa kupunguza umaskini na maendeleo ya kilimo na kukuza biashara.

Programu hizo ni jibu la hitaji la haraka la nchi za Afrika kwa maendeleo na zinalenga katika kuzisaidia kukuza uwezo wa maendeleo ya watu wa nyumbani, ambao ni kielelezo cha hivi punde zaidi cha ushirikiano wa vitendo kati ya China na Afrika na kukaribishwa kwa moyo mkunjufu na kuungwa mkono na upande wa Tanzania.

Programu hizo tisa zinatekelezwa nchini Tanzania kwa uthabiti na zikionekana katika;-

Kwanza, mwongozo wa kimkakati wa ngazi ya juu. Machi, mwaka huu, Mjumbe wa Taifa la China na Waziri wa Mambo ya Nje, Wang Yi, alifanya mkutano na Waziri wa Mambo ya Nje wa Tanzania, Liberata Mulamula. Pande zote mbili zilikubaliana kuimarisha ushirikiano chini ya mfumo wa FOCAC, kushinikiza utekelezaji wa programu tisa nchini Tanzania, na kuzalisha zaidi matokeo thabiti. Pande hizo mbili pia zinajadili kuhusu kufanyika kwa mkutano wa sita wa Tume ya Pamoja ya Uchumi na Biashara ili kuingiza nguvu mpya katika utekelezaji wa programu tisa.

Pili, mpango wa upande wa Kichina. Kwa mujibu wa matakwa mapya ya maendeleo ya hali ya juu ya ushirikiano kati ya China na Tanzania, nimekuwa na mikutano mingi na mawaziri wa afya, mawasiliano na elimu wa Tanzania ili kutengeneza upya urafiki kati ya China na Tanzania, kupanua ushirikiano baina ya nchi hizo mbili, hasa katika maeneo mapya ya afya, uchumi wa kidijitali, maendeleo ya kijani kibichi na maendeleo madogo ya hewa ya ukaa, na elimu ya ufundi stadi na kuhimiza uzinduzi na utekelezaji wa miradi midogo zaidi ya kujikimu kimaisha nchini Tanzania inayoweza kuwanufaisha wananchi.

Tatu, umuhimu unaowekwa na upande wa Tanzania. Tanzania sasa inatekeleza Dira yake ya Maendeleo 2025 na Rais Samia Suluhu Hassan ana mpango kabambe wa kuipa nguvu Tanzania, hivyo kuwa na matarajio makubwa katika ushirikiano wa kiutendaji kati ya China na Tanzania chini ya programu tisa. Kuanzia mwishoni mwa 2021 hadi Juni, mwaka huu, upande wa Tanzania umetoa matoleo mawili ya orodha ya miradi, ambayo inaonyesha umuhimu ulioambatanisha na programu tisa.

**SWALI**: Je, ni maendeleo gani ya hivi punde ya ushirikiano kwa vitendo kati ya China na Tanzania?

Kwa sasa, utekelezaji wa programu tisa nchini Tanzania umepata mavuno yake mapema. Kundi jipya la dozi milioni tatu za chanjo ya UVIKO- 19 zilizotolewa na China ziliwasili Tanzania Julai 14. Hadi sasa China imetoa dozi 5,610,000 za chanjo ya UVIKO-19 kwa Tanzania.

Kituo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma mkoani Kagera kilichojengwa kwa msaada wa China kimekamilisha kukubalika kwa mradi wa kiufundi na kitakabidhiwa kwa Tanzania hivi karibuni. Mradi wa Kitaifa wa Mapitio na Maendeleo ya Viwango vya Kazi ulizinduliwa Juni na China itashiriki katika ukuzaji wa viwango vya kazi na mipango inayohusiana ya kukuza vipaji.

Katika hatua inayofuata, China itadumisha mawasiliano na uratibu wa karibu na upande wa Tanzania, kuzingatia utekelezaji wa programu tisa, na kuwezesha uzinduzi wa miradi zaidi ya ushirikiano nchini Tanzania. China pia itaendeleza miradi midogo lakini yenye manufaa kama vile ushirikiano wa teknolojia ya Juncao ili kukuza maendeleo ya kiuchumi na kuboresha maisha nchini Tanzania na kufanya kazi kwa ajili ya kuendeleza na kuboresha ushirikiano kati ya China na Tanzania. Tutaungana mkono, chini ya uongozi wa Ari ya Tazara, kujenga jumuiya ya China na Afrika yenye mustakabali wa pamoja katika enzi mpya.

**SWALI:** Tukizungumzia urafiki wa China na Tanzania, mtu anaweza kukumbuka kwa urahisi Reli ya Tanzania-Zambia (TAZARA). Hivi karibuni, Rais Xi Jinping alisema tunapaswa kuendeleza ari ya TAZARA, tuiweke ilingane na mwenendo wa nyakati na kuifanya kuwa njia muhimu ya usafirishaji katika eneo la kanda hiyo. Kwa maoni yako, ari ya TAZARA ni nini? Nini kiini cha ari kwa kizazi kipya cha China na Tanzania?

**BALOZI CHEN:** Mjumbe wa Baraza la Taifa la China na Waziri wa Mambo ya Nje Wang Yi alifafanua ari ya Tazara mwaka 2015, ambayo ni kuhusu kuheshimiana na usawa, mshikamano na uvumilivu, na kujitolea kimataifa.

Ari ya TAZARA inajumuisha nyakati hizo za kukumbukwa za mazungumzo ya kirafiki kati ya China, Tanzania na Zambia. Ilijumuisha hadithi ya ziara 13 za Rais Julius Nyerere nchini China ambapo kupitia hizo alikuza urafiki wa kina na viongozi wa kizazi cha zamani wa China kama Mao Zedong, Liu Shaoqi na Zhou Enlai. Pia ilijumuisha hadithi ya zaidi ya watu 50,000 Wachina waliosafiri maelfu ya maili hadi Tanzania na kuunda urafiki wa kina kupitia kazi ngumu na kujitolea kwa ujenzi wa reli.

Hii ilijumuisha hadithi ya China kusaidia watu wa Kusini-mashariki mwa Afrika katika mapambano yao ya kujitenga na utawala wa kikoloni na kupata uhuru na ukombozi wa kitaifa katika miaka ya 1960. Ninaamini kwamba hadithi hizo za kukumbukwa, pamoja na Ari ya Tazara, zitakumbukwa daima katika historia ya mabadilishano ya kirafiki kati ya China na Tanzania na China na Afrika.

Tangu kukamilika kwake, TAZARA imesafirisha karibu tani milioni 30 za bidhaa na takriban abiria milioni 50. Licha ya takriban miaka 50 ya mabadiliko, TAZARA inafanya kazi leo, ikiwa na jukumu muhimu katika kuimarisha mawasiliano ya kikanda, kukuza maendeleo sawa ya kiuchumi na kijamii ya mikoa na kuleta urahisi kwa maisha ya watu. Muhimu zaidi ni kwamba, vizazi vipya vya China na Tanzania vimeipeleka mbele ari ya Tazara na kuiweka ilingane na mwenendo wa nyakati.

China na Tanzania siku zote zimekuwa zikifuata kanuni ya kuheshimiana na kushirikiana kwa mafanikio ya pamoja katika kuendeleza uhusiano wao. Nchi hizo mbili zimesaidiana katika juhudi zao za kutafuta kwa uhuru njia ya maendeleo inayofaa hali zao za kitaifa, na juu ya masuala yanayohusiana na masilahi yao ya kimsingi na masuala makuu.

China na Tanzania wote wanakabiliwa na kazi ngumu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Chini ya uongozi wa Chama cha Kikomunisti cha China (CPC), China imedumisha ukuaji wa haraka wa uchumi, na ujamaa wenye sifa za Kichina umeonyesha uhai wake mkubwa katika ardhi ya China. Kama chama tawala nchini Tanzania kwa miaka mingi, CCM inatekeleza Dira ya 2025 na kufanya kazi kwa bidii ili kuboresha miundombinu na maisha. Nchi hizo mbili zinafanya juhudi zisizo na kikomo kufikia matarajio ya watu ya maisha bora.

Kama mfano wa nchi zinazoendelea, China na Tanzania zinalinda kwa uthabiti mshikamano na maslahi ya pamoja ya nchi zinazoendelea katika masuala ya kimataifa, na kuunga mkono ushirikiano wa pande nyingi na jukumu la Umoja wa Mataifa.

Nchi hizo mbili zinafanya kazi pamoja na nchi nyingine kuchangia nguvu zao katika ujenzi wa jumuiya yenye mustakabali wa pamoja wa wanadamu. Nina imani kwamba ari ya Tazara ya kuheshimiana, mshikamano na uvumilivu, na kujitolea bila ubinafsi itang'aa kwa uzuri zaidi katika enzi mpya.

# Vietnam kujenga viwanda vya kubangua korosho

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimesema serikali inafanya mazungumzo na serikali ya Vietnam ili kujenga viwanda vya kubangua korosho na kuziongezea thamani badala ya kuiuza zikiwa ghafi.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Revocatus Rasheli, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa kongamano la kiuchumi baina ya Tanzania na Vietnam.

Alisema kwa muda mrefu Vietnam imekuwa ikinunua korosho ghafi kutoka Tanzania na kwenda kuziongezea thamani na kuziuza kwenye masoko ya nje, lakini serikali imeona ni wakati mwafaka sasa wa kuachana na utaratibu wa kuziuza zikiwa ghafi.

Vietnam, alisema imekubali ikianzisha viwanda vya kubangua korosho nchini kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi wa ndani ambapo wataziongezea thamani kabla ya kuiuza nje.

Alisema Vietnam ina miradi sita tu ambayo imesajiliwa TIC katika sekta za utalii, mawasiliano na ujenzi wa majengo yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.57 na kupitia miradi hiyo, imezalisha ajira 200,000 kwa Watanzania.

"Hawa wamesajili miradi michache tu lakini thamani ya miradi hiyo ni kubwa sana. Unaweza kukuta nchi imesajili miradi mingi lakini thamani yake ni ndogo lakini sisi tunacholenga zaidi ni ajira na kuvutia mitaji kutoka nje ya nchi," alisema Rasheli.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho, Francis Alfred, alisema Vietnam ni mnunuzi mkubwa wa korosho za Tanzania ikifuatiwa na India ambazo kwa pamoja zinachukua asilimia 90 ya korosho ghafi zinazotoka Tanzania.

Alisema Bodi ya Korosho imepanga kuongeza uzalishaji wa zao hilo hadi kufikia tani 700,000 kwa mwaka wa 2025/26 na kwamba kongamano hilo limewapa fursa ya kukutana na wanunuzi wa korosho ambao watajenga viwanda vya kubangua.

"Tuna changamoto ya kasi ya ubanguaji wa korosho kwa sababu tunabangua tani 63,000 tu. Viwanda vipo lakini hawabangui kiasi kikubwa na changamoto yao kubwa walikuwa wakisema ni upatikanaji wa malighafi lakini sasa tumewaruhusu wanunue moja kwa moja kutoka kwa wakulima," alisema.

Alisema soko la korosho ghafi ni dogo hivyo serikali inaweka mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji kuanzisha viwanda vya kubangua ili kuiongezea thamani ili iweze kuuzwa kwenye masoko mengi hali ambayo pia itaongeza ajira kwa Watanzania.

"Ukiuza korosho ghafi utauza India na Vietnam tu kwa sababu ndio wenye viwanda vya kubangua korosho, lakini ukiibangua utauza kwenye masoko ya Marekani, Russia, Mashariki ya Kati, Uarabuni na Marekani ndiyo sababu tumeona tuzungumze na hawa wanunuzi wakubwa wa korosho ghafi ili tuzibangue hapahapa nchini," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Ally Hapi (wa pili kushoto), akipata maelezo ya utendaji kazi wa mgodi wa Barrick North Mara, kutoka kwa Meneja Mkuu wa Mgodi huo, Apolinary Lyambiko (kushoto), alipofanya ziara ya kikazi mgodini hapo jana. Wengine ni wafanyakazi wa kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpelelezi aibua jambo bastola iliyotishia kuua

**Na Grace Gurisha**

SHAHIDI wa upande wa Jamhuri, kutoka Idara ya Upelelezi Mkoa wa Ilala, WP 2602 D/S/SGT Pendo (47), amedai katika Mahakama ya Wilaya Ilala, kwamba bastola iliyotumiwa na mfanyabiashara Adelade Lyakurwa (60), kutishia kuua hajailipia kwa kipindi cha miaka minne.

Lyakurwa anatuhumiwa kutishia kumuua kwa bastola mfanyabiashara Valence Matunda, Julai 30, 2020 maeneo ya Kariakoo, Mtaa wa Mbaruku na Swahili, Wilaya ya Ilala, huku akijua ni kinyume cha sheria.

Shahidi Pendo alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi, Groly Nkwera wa mahakama hiyo wakati akiongozwa na Wakili wa Serikali, Agatha Lumato, kutoa ushahidi wake katika kesi ya kutishia kuua kwa kutumia bastola.

Alidai Agosti 12, 2020 alikuwa ofisini, alipokea jalada kutoka kwa RCO la kutishia kuua kwa silaha ili aendelee na upelelezi na alipolisoma alibaini linahusu kutishia kuua kwa silaha aina ya bastola. Mlalamikaji katika kesi hiyo ni Valence Matunda.

Imedaiwa kuwa aliwasiliana na mlalamikaji ili kujua tukio kwa undani na mtu mmoja alijulikana kwa jina la Shabani, baada ya kuongea nao aligundua kuwa siku ya tukio Julai 30, 2020 mshtakiwa alikamatwa na askari wa Kituo Kikuu cha Polisi, lakini katika uchunguzi wake aligundua kuwa hakufikishwa katika kituo cha polisi.

Alidai wakati huo mlalamikaji na mashahidi maelezo yao yameandikwa na aliwasiliana na mshtakiwa kwa njia ya simu na kumtaka aende kituo cha polisi, lakini alidai hawezi kwenda kwa sababu yuko mbali.

Shahidi Pendo alidai kuwa siku ya pili alimpigia tena simu mshtakiwa huyo na kumweleza tuhuma zake za kutishia kuua kwa silaha na mshtakiwa alikubali kuwa anamiliki silaha.

"Nilimtaka aisalimishe kwangu silaha hiyo, aliniambia hakuja nayo kituoni ameiacha ofisini kwake, hivyo nilimwamuru Sajenti Selemani amwandike maelezo yake na kisha tuliondoka naye hadi mtaa wa Mbarouk ofisini kwake tulipofika alituongoza katika meza anayokaa na kusema silaha ipo kwenye droo."

"Nilifungua droo nikapata silaha aina ya bastola yenye rangi nyeusi, risasi tatu na kitabu cha bunduki baada ya kuvipata nilivijaza kwenye hati ya upekuzi na ni kasaini na mshtakiwa naye alisaini Agosti 13, 2020," alidai Pendo.

Shahidi huyo aliendelea kudai kuwa akiendelea na uchunguzi wake, Februari 15, 2021 aliandika barua kwenda kwa msajili wa bunduki Makao Makuu Dodoma akitaka kujua kama mshtakiwa huyo anaimiliki silaha hiyo kihalali.

"Tulipata barua ya majibu kuwa mmiliki halali ni Adelade Emmanuel Lyakurwa anaimiliki kihalali isipokuwa hajailipia ndani ya miaka minne, mara ya mwisho kuilipia ilikuwa mwaka 2017," alidai Pendo.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Julai 21, mwaka huu kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa.

# DC amaliza mgogoro utafiti wa mafuta

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MKUU wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, ametatua mgogoro wa wafugaji katika kijiji cha Magalata wilayani hapo wa kuzuia shughuli za utafiti wa mafuta.

Shirika la Maendeleo la Mafuta ya Petroli Tanzania (TPDC) linafanya utafiti kubaini uwapo wa mafuta katika Bonde la Eyasi Wembere ambalo limepita pia katika kijiji cha Magalata, eneo wanaloishi idadi kubwa ya jamii ya wafugaji kabila la Wataturu.

Mkude alisema juzi kuwa si vyema wananchi kupinga maendeleo kwa sababu utafiti huo ukikamilika na kubainika eneo hilo kuna mafuta, mradi huo utakuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo na kubadilisha maisha ya wananchi kiuchumi na taifa kwa ujumla kunufaika na mafuta hayo.

"Nimekuja kutoa elimu kwa wananchi na kutatua huu mgogoro wa kuzuia shughuli za utafiti wa mafuta hapa katika kijiji cha Magalata. Tatizo kubwa ambalo nimelibaini ni ukosefu tu wa elimu pamoja na kutaka kujua faida za huu mradi endapo mafuta yakipatikana," alisema Mkude.

"Mafuta yakipatikana eneo hili kwanza wananchi lazima mlipwe fidia kabla ya serikali kuitwaa ardhi hii na mtajengewa majumba mazuri pamoja na kutafutiwa sehemu nzuri ya malisho ya mifugo yenu. Pia mtawekewa huduma mbalimbali za kijamii ukiwamo ujenzi wa shule, hospitali, miundombinu ya barabara, na miradi ya maji," aliongeza.

Pia aliwasihi wafugaji hao kuruhusu shughuli za utafiti wa mafuta ziendelea kwa sababu hazizuii kuendelea na shughuli za kuchunga mifugo kwenye mbunga hiyo, hadi pale mafuta yatakapobainika kuwa yapo ndipo zitafanyika taratibu sasa za kisheria kuwa hamisha eneo hilo.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kishapu, Shija Ntelezu, aliwataka wafugaji hao waupokee mradi huo wa utafiti wa mafuta kwa sababu una maslahi mapana ya kiuchumi kwa taifa na kuwataka wapuuze maneno ya baadhi ya watu ambao wanawapotosha kwa maslahi yao binafsi, na hakuna mwananchi ambaye ataonewa bali kila mtu atapata haki yake.

Meneja Mradi wa Utafiti wa Mafuta Bonde la Eyasi Wembere kutoka TPDC, Sindi Maduhu, alisema utafiti huo wa mafuta katika bonde hilo ulianza mwaka 2015, na unafanyika katika mikoa mitano ambayo ni Arusha, Singida, Tabora, Simiyu, pamoja na Shinyanga.

Alisema shughuli ambazo wanazifanya kwa sasa ni uchukuaji tu wa sampuli ambazo baadaye zitapelekwa kwenye maabara nchini Marekani ili kupata majibu ya kubaini kama maeneo hayo yana mafuta. Alibainisha kuwa shughuli za utafiti huo wa mafuta hazizuii matumizi ya ardhi kuendelea kufanyika.

Mwenyekiti wa Wafugaji katika kijiji hicho, Kidonge Magulunga, alisema awali walizuia shughuli hizo za utafiti wa mafuta, sababu walishangaa kuona tu wageni wakifanya shughuli zao kwenye maeneo yao bila ya wao kuwa na taarifa, ndipo wakahofia huenda mbuga yao inataka kuchukuliwa na kuamua kuzuia utafiti huo.

Alisema kwa sasa baada ya kupata elimu na utambulisho rasmi, wamekubali shughuli hizo ziendelee za utafiti wa mafuta, na wapo tayari kushirikiana nao na kuwahakikishia ulinzi wa kutosha na hakuna ambaye atawasumbua tena wala kuwatishia maisha, bali watakuwa salama hadi pale watakapomaliza shughuli zao za utafiti.

# Bima maalum magari makubwa yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bima ya Phoenix Assurance imezindua huduma ya BimaPlus kwa wamiliki wa magari makubwa ya usafirishaji wa bidhaa mbalimbali ndani na nje ya nchi.

BimaPlus itawawezesha wafanya biashara hao kulipwa fidia ya bidhaa zao na gari husika endapo watapatwa na majanga mbalimbali, yakijumuisha ajali wakiwa njiani.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Ashraf Musbally, alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa lengo la huduma hiyo ni kulinda mtaji wa mfanyabiashara atakayejiunga na bima kubwa.

Musbally alisema wafanyabiashara wa bidhaa mbalimbali zinazokwenda mikoani au nje ya nchi, wanakuwa na wakati mgumu wakati mali zao zinaposafirishwa, wakiwa na maswali kama mzigo utafika salama kutokana na matatizo mbalimbali, ukiwamo wizi.

Alisema kuwa kupitia BimaPlus, mfanyabiashara atakuwa na uhakika wa mali zake pamoja na chombo cha usafirishaji.

"Kupitia BimaPlus, msafirishaji atakuwa na uhakika wa mali na mtaji wake kwani kampuni yetu itakuwa tayari kulipa fidia endapo kutatokea mali husika kupotea," alisema Musbally.

Alisema huduma hiyo ni muhimu kwa wafanyabiashara na kuwaomba kujiunga nayo kwa kuwa inalipa fidia kwa dereva, utingo, mmiliki wa mzigo na mwathirika wa tatizo na wategemezi wake.

"Uanzishwaji wa huduma ya BimaPlus ni mwendelezo wa ubunifu na upanuaji wa shughuli zetu katika soko la bima nchini.

"Lengo letu ni kumfaidisha mteja wetu na kuwa na amani katika shughuli zake. Kupitia BimaPlus, mteja wetu atakuwa na uhakika wa biashara yake kwa sababu mali zitakuwa salama na vilevile chombo cha usafirishaji. Kampuni yetu italipa fidia kwa majanga yoyote yatakayotokea," alisema.

Alibainisha kuwa huduma ya BimaPlus pia inamlipa fidia dereva na wafanyakazi wengine katika gari husika endapo watakuwa wamepata ajali.

Meneja wa Kanda ya Mashariki wa Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima (TIRA), Frank Fred, aliipongeza kampuni hiyo kwa kuanzisha bima hiyo ambayo inaleta suluhisho kwa wafanyabiashara wasafirishaji nchini.

Fred alisema bima hiyo inawapa uhakika wafanyabiashara wa sekta ambayo imekuwa na vikwazo kadhaa.

Alisema bima ya BimaPlus itachangia katika kujenga uchumi nchini na TIRA itaendelea kuunga mkono jitahada na ubunifu wa Phoenix Assurance katika kuleta maendeleo nchini.

Kamanda Msaidizi wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Kamishna Msaidizi wa Polisi Meloe Buzema, alisema bima hiyo inaleta chachu ya maendeleo ya sekta hiyo nchini.

"Ninawapongeza Kampuni ya Phoenix kwa kuanzisha bima hiyo ambayo inaleta faraja kwa wafanyabiashara wa usafirishaji na kuwajali madereva pia," alisifu.

# Wakili: Sheria uhalifu mtandaoni ni tishio, hatari kwa wanahabari

**Na Mary Geofrey**

SHERIA ya Uhalifu wa Mtandaoni imebeba maneno yenye ukakasi na yaliyo hatari zaidi kwa mwanahabari, imeelezwa.

Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA - TAN), Wakili James Marenga, alisema jana katika semina kwa waandishi wa habari za mtandaoni iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Wakili Marenga alisema sheria hiyo ina maneno hatari yanayoweza kumuumiza mwandishi wa habari kwa kiwango kikubwa.

"Tusipokuwa makini, sheria hizi zitaumiza wengi," alisema

Wakili Marenga huku akibainisha kuwa sheria hiyo imeweka baadhi ya maneno ambayo yanaweza kutumiwa vibaya na mahakama huku tafsiri yake ikiwa imefichwa.

Alitaja baadhi ya maneno yenye mitego katika sheria hiyo ikiwa ni pamoja na 'kwa namna nyingine' au 'kusudio na kinyume cha sheria.'

"Neno kama 'kwa namna nyingine ama kusudio na kinyume cha sheria,' ni maneno hatari yanayotumika hasa kuharamisha jambo ambalo si kosa kisheria. Maneno haya unaweza kuyaona kuwa ya kawaida lakini ni hatari sana," alisema.

Wakili Marenga alisema kwenye sheria hiyo kuna adhabu zilizowekwa kwa makosa ambayo hayapo wazi kinyume na Ibara ya 13 (6) (C) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema sheria hiyo kupitia Kifungu 7(i)(g) iliyotungwa mwaka 2015, imevuruga uhuru wa faragha taarifa binafsi za mtu zinaweza kuchukuliwa na Polisi kinyume na Ibara ya 16(i) ya Katiba ya Tanzania.

"Sheria hii katika Kifungu cha 50 (2)(b) inaondoa haki ya mtu kukata rufaa kinyume na Ibara ya 13(6) (a) ya Katiba, lakini pia Kifungu cha 38(2)(b) cha sheria hii kinaruhusu usikilizwaji wa shauri mahakamani hata bila muhusika kuwapo.

"Hukumu ikitolewa, ndio unatafutwa na kufungwa bila kujua kesi yako ilipelekwa mahakamani lini, na kwa kosa gani. Ndio maana tunasema sheria hii inatakiwa kupitiwa upya," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashidi Chuachua (katikati) na Mkuu wa Kitengo cha Mauzo na Usambazaji cha Kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, George Lugata, wakiteta jambo ndani ya duka linalotembea la Vodacom baada ya kulizindua katika eneo la Kabwe, jijini Mbeya jana. Kampuni hiyo, imedhamiria kufikisha huduma kwa wateja wake katika maeneo ambayo hayana maduka kwa kanda ya nyanda za juu kusini na hasa vijijini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ataka makandarasi wachangamkie fursa CRDB

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amewataka makandarasi na wazabuni nchini kutumia fursa za uwezeshaji zinazotolewa na Benki ya CRDB ili kuongeza ufanisi katika kazi zao na kuwajengea uwezo wa kushiriki kikamilifu katika miradi ya kimkakati nchini.

Prof. Mbarawa alitoa rai hiyo jana alipofungua Kongamano la Uwezeshaji kwa Makandarasi na Wazabuni lililoandaliwa na CRDB jijini Dar es Salaam.

Waziri huyo alisema fursa hizo zitasaidia kupunguza kero za ucheleweshwaji wa miradi mbalimbali kutokana na kukosekana kwa mtaji.

"Benki ya CRDB imewaletea fursa mlangoni, itumieni kupata mitaji nafuu kujijengea uwezo utakaowawezesha kushiriki kikamilifu katika miradi," alisema Prof. Mbarawa huku akibainisha kuwa uwezeshaji huo unaofanywa na CRDB utasaidia kutimiza azma ya serikali ya kuhakikisha makandarasi wazawa wanashiriki katika miradi (local content).

Prof. Mbarawa aliipongeza CRDB kwa kuwa mstari wa mbele katika kuunga mkono juhudi za serikali katika miradi ya ujenzi wa miondombinu mbalimbali nchini ambayo itasaidia kuchochea ukuaji wa uchumi.

"Tunatambua na kuthamini sana ushikiri wa CRDB katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati nchini. Asanteni na hongereni sana," alipongeza.

Prof. Mbarawa aliishauri CRDB kupunguza riba katika mikopo ya makandarasi kama ambavyo imekuwa ikifanya kwa sekta zingine, ikiwamo ya kilimo, ili kuwajengea uwezo makandarasi na kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika miradi inayotekelezwa na serikali.

"Tunawapongeza kwa mikopo hii isiyo na dhamana na maboresho mengine mliyofanya, lakini niwaombe mpunguze riba ili kutoa unafuu zaidi. Vilevile, nitoe rai kwa makandarasi kurejesha mikopo kwa wakati kama ilivyo katika makubaliano," alisema.

Prof. Mbarawa pia akiishauri benki hiyo kuisaidia serikali kutoa mafunzo ya usimamizi wa miradi kwa makandarasi na wazabuni.

Waziri huyo pia alipongeza uamuzi wa benki hiyo kufungua kampuni tanzu katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), akisema uamuzi huo utasaidia kufungua fursa nyingi kwa wafanyabiashara nchini ikiwamo makandarasi na wazabuni.

"Congo kuna uhitaji mkubwa wa miundombinu ya barabara na nchi zetu zimekuwa katika mazungumzo ya namna gani tunaweza kusaidia katika kuboresha eneo hili hasa ukizingatia biashara baina ya nchi zetu inaendelea kukua," alisema na kuipongeza CRDB kwa kutunukiwa tuzo ya Benki Bora Tanzania na jarida la Euromoney la Uingereza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alimhakikishia Prof. Mbarawa kuwa benki yao kupitia kaulimbiu yake ya "Tupo Tayari", imejipanga vilivyo katika kuhakikisha inashirikiana na serikali kuboresha miundombinu nchini ili kufungua fursa za kiuchumi na kuvutia wawekezaji.

Nsekela alisema CRDB imefanya maboresho katika huduma zake inazotoa kwa kundi hilo ambapo hivi sasa makandarasi wakubwa na wadogo watawezeshwa kupata huduma za mikopo bila dhamana yoyote.

Alisema baadhi ya huduma zilizofanyiwa maboresho ni pamoja na dhamana ya zabuni 'Bid bond', dhamana za utekelezaji wa miradi 'Performance Guarantee', dhamana za malipo ya awali 'Advance Payment Guarantee' pamoja na huduma za mikopo ya mitambo.

Nsekela aliongeza kuwa benki hiyo pia imeboresha taratibu zake za utoaji mikopo na hivyo kuwashauri makandarasi kujitokeza kwa wingi kuomba mikopo, kufungua akaunti pamoja na kujiunga na huduma za bima ili kujikinga na majanga yanayoweza kutokea.

"CRDB ni benki yenu, niwahakikishie tu sisi tupo tayari kuwahudumia," alihitimisha Nsekela.

Akizungumza kwa niaba ya makandarasi na wazabuni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Ukandarasi ya Gopa Contractors Tanzania Ltd, Godfrey Mogellah, aliipongeza CRDB kwa hatua hiyo ya kuwakutanisha wadau wa sekta ya ujenzi nchini.

Alisema fursa zinazotolewa na Benki ya CRDB, zitakwenda kuleta sura mpya katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu nchini.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kushoto), akizungumza na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, Mark Bryan Schreiner, katika maadhimisho ya Siku ya Idadi ya Watu Duniani yaliyofanyika kitaifa, wilayani Hanang', mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mil. 998/- kuboresha maeneo ya wazi

**Na Faustine Feliciane**

WILAYA ya Temeke imetenga Sh. milioni 998 kwa ajili ya kuendeleza maeneo ya wazi na upandaji miti 1,927 ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Akizungumza jana na waandishi wa habari alipotembelea eneo la wazi la Mwembeyanga, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, alisema mradi huo ni sehemu ya lengo la mkoa wa Dar es Salaam kuboresha maeneo yake na kuyafanya kuwa ya kijani (Green Dar).

Mwegelo alisema mradi umeshaanza kwa kuboresha maeneo ya Mwembe Yanga kwa kujenga viwanja vya michezo, upandaji miti na maua, ukarabati wa mifereji kwenye baadhi ya barabara.

Kazi zingine ni kupanda maua kwenye mfereji wa Serengeti na kandokando ya barabara ya Mtoni Kijichi kuelekea Toangoma ndani ya wilaya hiyo.

"Kuhusu upandaji wa miti, alisema miti 1,427 itapandwa na halmashauri, maeneo ya wazi miti 500 watapewa wananchi kwenda kupanda kwenye maeneo yao," alisema.

Pia alisema Manispaa ya Temeke inatekeleza kwa vitendo maagizo ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, ya kutaka Dar es Salaam kuwa safi na maeneo ya wazi ya kupumzika wananchi.

"Sasa pamoja na usafi tunaofanya, uwapo wa maeneo haya ya wazi yakiwa kwenye ubora mzuri si tu tutapendezesha Jiji, lakini tutakuwa tumewapa wananchi maeneo ya kupumzika," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kutunza mazingira na miundombinu hiyo ili iwe endelevu kwa faida ya sasa na baadaye.

Naye mratibu wa mradi huo ambaye pia ni Meneja wa Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA), Manispaa Temeke, Mhandisi Paul Mhere, alisema mradi huo umefikia asilimia 25.

Alisema baada ya kukamilika ujenzi wa maeneo hayo ya wazi yatakuwa chini ya halmashauri, lakini wananchi watatakiwa kulipia wanapotumia.

"Kwa wale waliokuwa wakikodi maeneo haya kwa ajili ya shughuli za biashara au nyingine, wataendelea kufanya hivyo kwa utaratibu wa manispaa na maeneo haya sasa yatakuwa chini ya uratibu wa manispaa," alisema Mhere.

Naye msimamizi wa mradi huo kutoka kampuni ya ujenzi ya Group Six International, Seleman Hamduni, alisema mradi huo utakamilika baada ya miezi miwili.

# Vyuo vikuu India, Georgia kufungua matawi Dar

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu cha Sharda cha India na GEOMEDI cha Georgia, vimepanga kuanzisha matawi nchini baada ya kuvutiwa na mazingira yaliyoko ya uwekezaji kwenye sekta ya elimu.

Wawakilishi wa vyuo hivyo, waliyasema hayo jana kwenye banda la Global Education Link (GEL) wakati wa Maonyesho ya Vyuo Vikuu yanayoendelea kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam.

Meneja Masoko wa Chuo Kikuu cha Sharda, Mudasir Naik, aliliambia gazeti hili kwamba chuo hicho kimeonyesha aina ya kozi kinazotoa na Watanzania wengi wameonyesha kuvutiwa.

Alisema maonyesho hayo yamekuwa na manufaa makubwa kwa chuo hicho kwa kuwa wanafunzi wengi wamekuwa wakitembelea kujua aina ya kozi wanazotoa, hivyo wameonyesha kupenda kujiunga nacho siku za usoni.

Naik alisema chuo hicho kimekuwa kikipokea wanafunzi kutoka mataifa mbalimbali na kwa Tanzania kuna zaidi ya wanafunzi 150 ambao wanaendelea na masomo kwenye chuo hicho ambacho kimetajwa na mamlaka za nchi kuwa miongoni mwa vyuo 10 bora nchini India.

"Tuna kila aina ya vifaa vya kutoa mafunzo ya uhandisi, teknolojia, biashara, sayansi ya kompyuta, uchambuzi wa data, kumwezesha mwanafunzi anayesoma Sharda hapa kwenda kufanya kazi tena kwa ufanisi mkubwa popote pale duniani," alisema.

Aliipongeza Global Education Link (GEL) kwa namna ambavyo imekuwa ikiwaunganisha wanafunzi wa Tanzania kusoma kwenye vyuo mbalimbali vya nje ya nchi na kwamba asilimia kubwa ya wanafunzi wanaosoma kwenye vyuo vya India wamepitia kwa wakala wa GEL.

Naye Irene Shadari ambaye ni Mdhibiti Ubora wa Chuo Kikuu cha GEOMEDI, Georgia alisema chuo hicho ni miongoni mwa vyuo vilivyofanikiwa zaidi nchini humo kwa kutoa elimu bora inayomwezesha mwanafunzi kujiajiri.

Alisema wanatoa kozi za maabara, meno, tiba ya afya, uchumi wa afya, utabibu, tiba kwa magonjwa ya akili na wasomi wa kada mbalimbali za sekta ya afya.

Shadari alisema mwanafunzi anayesoma kwenye chuo hicho anafundishwa nadharia ya kutosha na kupewa mafunzo ya vitendo ya hali ya juu yanayomwezesha kwenda kufanya kazi kwa umahiri mkubwa kwenye taasisi zinazotoa huduma za afya.

"Elimu inayotolewa na chuo chetu inafuata viwango vya Ulaya na tunashirikiana na taasisi na vyuo vya kimataifa katika tafiti mbalimbali ambazo zinatuwezesha kufanikisha miradi ya kimataifa," alisema Irene.

Alisema chuo hicho kilianzishwa mwaka 1998 na Prof. Marina Pirtskhalava ambaye mwaka 2001 alitambuliwa kama mwanamke mwenye ushawishi mkubwa wa karne ya 21 na anafundisha lugha za Georgia, Kingereza na Kirusi na kimekuwa kikipata tuzo mbalimbali kutokana na kufanya vizuri kwenye taaluma na tafiti mbalimbali.

Vyuo kutoka mataifa mbalimbali vinahudhuria maonyesho hayo chini ya mwavuli wa GEL zikiwamo Iran, India, Georgia, Cyprus, Uturuki, Marekani, Uingereza, Mauritius, Dubai, Poland, Australia, Canada na Malaysia.

Vyuo vikuu vinavyoshiriki kwenye maonyesho hayo ni pamoja na Chuo Kikuu cha MM, Sharda, CT, Geomedi, GELISM, Lovely Professional University, LPU, PDEU na GNA.

# UDSM kuandika kitabu cha historia ya Tanzania

**Na Gwamaka Alipipi**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Ndaki ya Insia, Idara ya Historia (CoHU) kinaandaa kitabu kitakachoeleza historia ya Tanzania baada ya uhuru katika nyanja mbalimbali ikiwamo uchumi, elimu, utawala bora, maendeleo vijijini pamoja na mila na tamaduni za Watanzania.

Akizungumza wakati wa maandalizi ya kitabu hicho jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. Willium Anangisye, alisema uandishi wa kitabu hicho ni wa kwanza kufanywa na Watanzania kulinganishwa na vitabu mbalimbali vinavyoelezea historia ya Tanzania vilivyoandikwa na wageni.

"Walioshiriki katika kuandika kitabu hicho ni Watanzania. Kitabu kitaeleza matukio mbalimbali yaliyotokea nchini baada ya uhuru. Awali wageni ndiyo walikuwa wanaandika historia ya nchi yetu wakati wa ukoloni, lakini kwa sasa tunakwenda kuandika wenyewe," alisema Prof. Anangisye.

Alisema kuandikwa kwa kitabu hicho kutakuwa sehemu ya kumkumbuka aliyekuwa profesa wa kwanza wa somo la historia nchini, Prof. Isarian Kimambo.

Mhadhiri Mwandamizi wa UDSM kutoka Idara ya CoHU, Dk. Salvatory Nyanto, alisema maandalizi ya kuandika kitabu hicho yalianza mwaka 2020.

Dk. Nyanto alisema: "Maprofesa, wahadhiri wa kitanzania ndiyo walioshiriki kuandika kitabu hicho na ifikapo Agosti mwakani kitakuwa tayari kimechapishwa.

"Kuna vitabu vingi vimeandikwa kuhusu historia ya Tanzania vikielezea mambo mbalimbali yaliyofanyika kabla ya kupata uhuru, lakini hiki kinaenda kuzungumzia matukio yaliyotokea baada ya uhuru. Idara ya CoHU inakwenda kutimiza miaka 60 tangu ilipoanzishwa."

Mkuu wa Idara ya CoHU, Dk. Hezron Kangalawe, alisema kupitia kitabu hicho, Watanzania watafahamu namna sherehe za uhuru zilivyokuwa, watu walivyosherehekea na maandalizi yake.

Alisema Watanzania pia watafahamu chapisho la kwanza la gazeti la serikali lilikuwa na habari gani na lilikuwaje, kwamba matukio mbalimbali yaliyotokea baada ya uhuru yatakwenda kuwekwa katika kitabu hicho.



Tujikite kuzama na tafakari yenye mashiko, hitaji la leo




BUFE
IJUMAA JULAI 22, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Soko pana EAC na kuweka sawa usalama, kuna maana gani kwa biashara, uwekezaji?

**Na Peter Orwa**

JANA Rais Samia Suluhu Hassan, alikuwa mwenyeji katika mkutano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), jijini Arusha ambako ndio makao makuu ya chombo hicho, ambacho kilimkaribisha mgeni mpya kutoka taifa la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Hapo kuna wenyeji kuanzia na waasisi; Tanzania, Uganda na Kenya, pia Rwanda, Sudan Kusini na Burundi na ajenda mojawapo muhimu ni kwao soko la pamoja.


Kimsingi, ni aina ya ajenda inayomgusa moja kwa moja Rais Samia Suluhu Hassan, katika kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja madarakani, hata akajikuta anapewa sifa katika lugha "anaupiga mwingi'.

Ikirejewa utawala nchini na hasa ajenda ya chama tawala CCM, falsafa yao ya utekelezaji kati ya kiongozi mmoja na mwingine au awamu moja na nyingine ni dhana ya 'kupokezana kijiti.

Hiyo ndiyo maana hata juzi Rais kateua Inspekta Jenerali (IGP) mpya wa Polisi Camillus Wambura, wanapokezana kijiti na mtangulizi, Simon Sirro. Anayechukua nafasi, anaendeleza alikoishia mtangulizi na kwa maana hiyo, Rais Samia anasimamia hapo, kuendeleza mema ya watangulizi wake, huku akiboresha na mapya ya kwake.

Ni katika mtazamo huo, Rais Samia, kama walivyo watangulizi ana yake ambayo yanamtambulisha kwa upekee na mambo ya pamoja, hapo Rais Samia naye aking'ara na yake ya utendaji na nafasi yake, ikiwamo Rais wa kwanza mwanamama.

Pia, ana mengi chanya kutoka kwa wanaotakia heri jinsia ya kinamama, hata mashabiki wake hawakumchelewesha kumpatia uchifu - Hangaya, kwa hilo na ufanisi wa utendaji wake ofisini


Safu ya uongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mkutanoni, ambao himaya zao za uongozi, ni soko rafiki kwa wafanyabiashara wa nchini. **PICHA: MTANDAO.**

Hapo katika kipengele ofisini, nako kuna mengi yake. Kwa nafasi ya pekee, kama maandiko matakatifu hutamka 'utamuona kwa maneno na matendo yake."

Ndani ya muda wa uongozi wake, Rais Samia, amekuwa akipigana kuunda Tanzania salama yenye ishara ya upendo, amani na maendeleo ikiwa na biashara na uwekezaji unaokua kwa kasi kuzalisha ajira na kipato kwa wingi, ikiwa dira inayotawanyika katika fikra na mboni ya macho, pia ubongo wake.

Juzi wakati wa kumuapisha IGP Wambura, akathubutu kuweka wazi baadhi ya mambo ikiwamo haja ya kuwapo maboresho makubwa ya kimuundo na utendaji katika vyombo vya usalama, ikiwamo Polisi aliko Wambura na Magereza, akifanya hatua.

Hiyo maana yake nini? Kuboresha mazingira wezeshi kwa maendeleo, kupitia amani na haki kwa umma, ili Watanzania watetee amani, ajira na kipato chao kupitia uwekezaji na biashara.

Wakati yuko katika kikao cha EAC kinachoendelea jijini Arusha, ujumbe huo pia unapenya kupitia ajenda aliyoianika juzi, wakati wa kumuapisha IGP mpya.

Kundi kubwa la wananchama hao, ni soko la wazi kwa wawekezaji na wafanyabiashara nchini katika uchumi huo, ikizingatiwa ajenda mbele yake ni Soko la Pamoja' , baada ya kukidhi soko la nchini, sasa wanakuwa na fursa kutanua soko lao.

Hata hivyo katika upande wa pili wa shilingi, haina maana kwamba Watanzania hawajaanza kulitumia soko hilo. La hasha! Nchi jirani kama mgeni wa jumuiya - DRC, tayari wafanyabiashara na wakulima wa Tanzania wamekuwa wakiitumia kama soko lao, zikiwamo bidhaa za vyakula shambani.

Ni wiki hii, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ambaye katika kipindi kilichopo wizara yake imeidhinishiwa kiasi kikubwa sana cha fedha, ametamka mjini Morogoro namna serikali inavyowaandalia mazingira wezeshi ya uuzaji mazao yao, huku serikali ikiwasimamia kuwalinda.

**KUTOKA EAC**

Hiyo ina maana gani, kwa kurejea na kinachoendelea kupitia kikao cha EAC kilichoanza jana? Ajenda ya 'Soko la Pamoja' inamaanisha wakati wana jumuiya wakikaribishana kufanya biashara ya pamoja, wafanyabiashara nchini nao warejee kinachopiganiwa na Mama wa Taifa - Chifu Hangaya.

Ni fursa kwa wauza mazao kwa mfano, ni wakati wao kubeba ajenda hizo, kisha wanashirikiana, vilevile 'kumsumbua' Waziri Bashe na mwenzake, mchumi Dk. Ashatu Kijaji, wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji, eneo lenye unasaba na elimu ya Bashe.

Wanachofanya timu hiyo, ndio hisia ya Rais Samia, kwani ndio sehemu ya kikosi kazi kinachomtumikia katika sekta tofauti. Ufunguaji mlango huo si mgeni kibiashara, ikirejewa hata huko nyuma Rais Samia, alishafunga safari na kwenda kuonana na mwenzake, Rais Uhuru Kenyatta.

Zao la kukutana kwao ilifunguliwa milango ya biashara kwa kuondoa vikwazo kadhaa, vikiwamo vya mpakani na biashara inamea mpaka sasa, huku katika kipindi kingine kama hicho kilishuhudiwa nchini Uganda, katika sura ya mafanikio ya soko na uwekezaji.

Mara zote, kupanuka kwa soko nchini kuna maana kubwa kiuchumi, ikianza na ajira, kufungua milango zaidi ya Tanzania kuwa na mazingira wezeshi ya uwekezaji viwanda, kwa maana ni mzizi wa soko la bidhaa zake.

Hiyo ikioanishwa na maboresho aliyoyataja juzi katika eneo la Ulinzi na Usalama, inaangaliwa kwamba Tanzania inabaki kuwa mahali rafiki katika uwekezaji kimataifa.

Mtu anaweza kurejea matunda na safari zake katika nchi za kigeni kuandaa uwekezaji na biashara ya nchi, ambako kote ama akiwa huko ughaibuni au anaporejea, amekuwa na utaratibu kuwasilisha takwimu za kilichovunwa katika maeneo kama soko na uwekezaji, jibu likiangukia 'anaupiga mwingi'.

UCHUMI

MJUE MAMA BHOKE...

# Asimulia jinsi alivyokimbia ukatili katika ndoa Tarime, sasa muwekezaji mdogo Dar

•Akwea umaarufu wa kuuza mboga, ana kwake, 'maisha yanaendelea'

**Na Sabato Kasika**

MTU anaweza kudhani kuwa ni tamthilia, pale anaposimuliwa matukio katika maisha yake, lakini halisi ambayo yalimkuta Mama Bhoke Mussa, katika ndoa yake.

Huyu anatoka kijiji cha Bunge'eng'e wilayani Tarime mkoani Mara Kaskazini Magharibi mwa Tanzania, ambaye anasema kabla ya miaka 25 iliyopita, alipitia machungu mengi katika ndoa.

Bhoke ambaye amekimbia ndoa, wajihi wake ni mfupi, mwili wa wastani, maji ya kunde, lakini pia mchangamfu, ila tatizo lake ni kutojua Kiswahili vizuri, anazungumza huku akichanganya na kikurya.

Kwa sasa analima bustani za mboga, Mtaa wa Amani, Kata ya Kipunguni Dar es Salaam. Kadri anavyoisimulia Nipashe, ndivyo ninavyotamani kumfahamu zaidi, hasa baada ya kugusia suala la kukimbia ndoa.

Kutokana na maelezo hayo, ninamuomba azungumze na anakubali kufanya hivyo ndipo anasimulia alivyokuwa anapigwa na mume wake aliyekuwa na wivu kupita kiasi.



Bhoke (kushoto) akiwa katika bustani yake akichuma mboga na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk.Dhorothy Gwajima.

### KISA NA MKASA?

Bhoke anaanza kwa kueleza kuwa, nyumbani kwao walizaliwa watoto 12, wa kiume watano, wa kike saba, lakini sita wameshafariki dunia, wamebaki sita, wa kiume mmoja na wa kike watano, huku yeye akiwa wa mwisho kuzaliwa.

Hata hivyo, sura inaonyesha kusikitika anaposema kuwa nyumbani kwao wote hawakusoma, sababu ikiwa ni mila na desturi za jamii hiyo za kutoona umuhimu wa elimu zaidi ya kujali mali kwa kuoza mabinti.

Anasema, baada ya kupevuka, alikeketwa kisha baada ya kupona aliolewa, ambapo katika ndoa yake alibahatika kupata watoto wawili wa kike ambao nao anadai kuwa hawakusoma kama yeye.

"Mume wangu alikuwa mlevi na mwenye wivu, kila akitoka kulewa alikuwa ananipiga akidai nina wanaume. Siku moja saa tano usiku, alirudi na kunikuta nimelala na akaanza kuniuliza mambo ya wanaume, kisha akafuata sime katika uvungu wa kitanda," anasema.

Anasimulia wakati anachukua sime chini ya uvungu wa kitanda, ndipo yeye (Bhoke) akakimbia ikawa bahati yake, mlango ukiwa wazi na kwenda mji wa jirani kujificha na siku iliyofuata aliamua kwenda nyumbani kwao kuepuka mateso.

"Baada ya kufika kwetu, nikaagiza mabinti zangu wanileteе nguo, nikatafutiwa nauli na ndugu zangu kesho yake nikaondoka kuja huku Dar es Salaam ambako nimeanza maisha mapya," anasema.

### ATUA DAR ES SALAAM

Mwaka 1997 ndio ambao anasema alitua jijini Dar es Salaam, siku chache baada ya kukimbia mateso ya mumewe na kwamba baadaye alihudhuria mikutano ya utoaji wa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia.

"Elimu hiyo ilikuwa inatolewa na wanachama wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni ambao walikuja mtaani nilikofikia, nikavutiwa kuwasikiliza kisha nikaomba kufika ofisini kwao kuelezea yaliyonikuta," anasema.

Anasema, alikaribishwa na ndipo baada ya siku chache akaenda kuelezea kisa na mkasa, akachukuliwa na kuwa miongoni mwa wanawake waliokuwa wakifundisha ujasiriamali wa kituo hicho.

"Baada ya mafunzo ya viongozi wa Sauti ya Jamii, walinipa matuta 24 ya bustani, mbegu na mbolea nikaanza kulima mboga. Mauzo ya mwanzo nilichukua fedha nikawatumia mabinti zangu nauli wakaja huku," anasema.

Anasema, binti mkubwa kwa sasa ameolewa na kupata watoto sita, huku mwingine akiwa hajaolewa, na kwamba wawili hao wamekuwa wakimsaidia kufanya kazi katika bustani.

"Nimeajiri kijana anayenisaidia kulima na kumwagilia bustani zangu, maisha yanakwenda kama kawaida, nimeshasahau maisha ya ukatili wa kijinsia niliopitia wakati nikiwa katika ndoa," anasema.

Anaeleza kuwa kupitia uuzaji wa mboga, amefanikiwa kujenga nyuma ya kawaida ya vyumba viwili na amekuwa akipata Sh. 50,000 hadi 100,000 kwa siku kupitia mauzo ya mboga hizo pale soko linapokuwa zuri.

### MAISHA YA TARIME

Anasema maisha ya kijijini kwao ni magumu, binafsi anaona bora aendelee kuwekeza kupitia bustani za mboga za majini ili ikiwezekana apanue miradi yake zaidi au kubadili biashara aanzishe duka la vyakula.

"Kule kijijini hata kuvaa viatu ilikuwa ni shida, nilikuwa ninavaa mabondo ambayo yanamaliza wiki chache yameisha, hata nguo zilikuwa chakavu, kwa sababu sikuwa na za kubadilisha," anasema.

Bhoke anasema, hata mtu akiumwa alikuwa anachumiwa majani ya miti yanachemshwa kisha anafukizwa, iwapo majani hayo yataendana na ugonjwa, basi mtu anaweza kupona.

"Maisha hayo yamepitwa na wakati na sasa ni muhimu kwenda hospitali kupata vipimo kwanza kabla ya tiba. Sikusoma, lakini hilo kwa sasa huwezi kunidanganya, ninalijua," anasema.

### HALI ILIVYO NCHNI

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, anasema asilimia 40 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 hadi 49 nchini, wanadaiwa kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kimwili au kingono mara moja au zaidi katika kipindi chao cha maisha.

Aidha, anasema asilimia 20 ya wanawake wa umri kati ya miaka 15 hadi 49 wamefanyiwa ukatili wa kimwili katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, huku asilimia tisa ya wanawake wa umri kati ya miaka 15 hadi 49 wakiwa wameingiliwa kimwili bila ridhaa yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, anatoa wito kwa Jeshi la Polisi kuhakikisha linafanya upelelezi ili kubaini vyanzo vya ukatili huo kwa wanawake na kuchukua hatua stahiki kwa wote waliohusika.

Anasema, Tanzania imetia saini mikataba ya kimataifa, ukiwamo Mkataba wa Kupinga Aina Yoyote ya Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW).

Pia ataja Mkataba wa Nyongeza wa Haki za Wanawake wa Afrika (Maputo Protocol), kuwa mikataba yote ina vifungu vya kutetea na kulinda haki za wanawake.

Msaikolojia Roselighty Ringo wa asasi isiyo la kiserikali ya utoaji wa elimu kwa jamii na mambo yote ya saikolojia ya Empowerment (CYPE) anafafanua.

"Unaweza kuwa ukatili wa kingono, ukasababisha magonjwa kama UKIMWI, lakini pia kuna ukatili wa vipigo, unapokuja katika suala la athari kisaikolojia unaweza kukuta zinafanana," anasema Roselighty.

Anataja athari hizo kuwa ni manusra, kutojiamini, kutoamini watu, kutojikubali, ambapo mazingira kama hayo, anatakiwa kukutana na watu wa saikolojia, ili kuzungumza naye, kumshauri na kumuweka sawa.

"Ukatili wa kijinsia una madhara mengi, matokeo yake ni mabaya kwa wanawake na watoto, kwani yanaweza kudumu katika kipindi chote cha maisha ya manusura kama hakupata msaikolojia kumuweka sawa," anasema.



Bhoke akiongozana na Waziri Dk.Dhorothy Gwajima baada ya kumaliza kuchuma mboga. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tujikite kuzama na tafakari yenye mashiko, hitaji la leo




**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

MIAKA ya sabini, bila shaka 1973, Serikali ya Tanzania ilitangaza azma ya kuhamisha makao makuu ya nchi kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma. Hizo zilikuwa enzi za Rais wa Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere.

Watanzania waliambiwa uamuzi huo ulitokana na mikoa mingine kuwa mbali na Dar es Salaam, hususan lilipokuja suala la mikutano, hata wajumbe walilazimika kutoka mikoani kwenda Pwani.

Hivyo, ilionekana kuwa ni gharama kwao katika sekta hiyo ya mawasiliano, hususan ya barabara, hivyo ikasemekana kwa kuwa Dodoma ni katikati ya nchi, ingekuwa nafuu kwa wajumbe wote wakiwamo wa Kigoma, Dar es Salaam, Ruvuma na Mara.

Wananchi walishangilia uamuzi huo, na hata Mwalimu Nyerere katika kuonyesha mfano, akajenga Ikulu, Chamwino, Dodoma, ikiwa pia ni sehemu ya kuonyesha dhamira ya dhati ya kutekeleza uamuzi huo,ulioonekana kuwa na tija.

Ikaanzishwa Wizara ya Kusimamia uamuzi huo ikifuatiwa na Mamlaka ya Uendelezaji Makao makuu hayo, majengo ya wizara kadhaa yakajengwa Dodoma, mji ukaanza kubadilika taratibu kimandhari, angalau kuonekana makao makuu hivi, lakini baadaye likawa jiji!

Baada ya hapo ikawa kimya. Hatimaye, alipoingia Dk. John Magufuli, akasimamia kidete, watu wakahamia Dodoma kama safu, Dodoma ikajengwa kama kichuguu kwa kasi ya mchwa, hatimaye Dk. Magufuli mwenyewe akaibadilisha Chamwino kwa majengo likiwamo jengo pacha na la Ikulu ya Magogoni.

Leo watu wako Dodoma, waliobaki wachache wanahimizwa kuhamia, na watahamia,ili sasa tusahau ya Dar es Salaam na kubakiwa na makao makuu ya nchi Dodoma. Hapo sasa hakuna kurudi nyuma, lakini ilichukua muda gani? Miongo mitano na ushei!

Lakini, ukifikiria kwa kina zaidi, kilichokwamisha ni maendeleo tu, kwani sababu zilizokuwapo enzi zile za kuhamia Dodoma, leo zimekuwa nafuu, kama ni gharama za usafiri barabarani nzuri, pia mawasiliano ni rahisi, si lazima kutoka mahali kwenda kwingine kufanya mikutano!

Magufuli anaendelea kumuenzi Mwalimu Nyerere, hata akahamasika kufufua ujenzi wa bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere, ambalo aliliacha likiitwa Stiegler's Gorge.

Tuyaache hayo, hivi sasa kuna jambo lilibuniwa mwaka 2004 likazimia, lakini naona linapepewa ili lizinduke na liendelee.

Lipo hili suala la Vazi la Taifa. Limeanza tena kusumbua akiliza watu kama ilivyokuwa mwaka 2004 lilipoanzishwa na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo wakati huo, Emmanuel Nchimbi. Watanzania wanataka kuwa na vazi la Taifa!

Timu iliundwa kupata mawazo ya watu ilikuja na vazi hilo, wapo waliofikia kupendekeza eti khanga ingefaa, kwani inavaliwa na Watanzania wengi!

Kwa kifupi wazo hilo nalo lilionekana sawa na la kuhamisha makao makuu kwenda Dodoma.

Najiuliza, nini sababu ya kuwa na vazi la Taifa leo kweli? Kuna haja ya kufanya utafiti wa kina kuja na jibu pana zaidi. Watu pia wana ajenda ya kibaba cha mchele au mahindi, au sukari na mafuta ya kula na ya mitambo.

Tufikirie kwa kina, vazi la Taifa lina mengineyo kwa sura ya utafiti kujua utashi wao. Mpaka sasa huwa nawaona wabunge wana kanuni za mavazi yao ikiwamo kinamama suti na tai.

Ni kweli vazi lina nafasi, pia tufikirie kwa kina matatizo mengine ya msingi, hususan ya kupambana na ujinga, umasikini na maradhi na kadhalika.

Inapendeza tuende na upepo na muktadha uliopo duniani. Tuzame kudhibiti wanaoenda na mavazi yasiyo na staha kwenye mikusanyiko, ikiwamo ya harusi.

Wizara yenye dhamana ina kazi kubwa ya kufanya hapo. Alamsiki!

## BIASHARA

### CHEREKO KILIMO BIASHARA SAME...

# Wizara Kilimo rasmi yaingilia uboreshaji miundombinu ya kumwagilia tangawizi

### •Mbunge Kilango 'mguu kwa mguu' na mradi

**Na Mary Mosha, SAME**



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Umwagiliaji Taifa, Mhandisi Raymond Mndolwa, akiwa na Mhandisi wa tume hiyo mkoani Kilimanjaro, Said Ibrahim (aliyevaa koti jeusi) na Diwani wa Kata ya Mamba Miamba (aliyevaa Sweta), Greyson Kiondo. **PICHA ZOTE: MARY MOSHA.**

TANGAWIZI ni zao la kiungo, linalotumika kama kitunguu na ina asili ya maeneo ya kitropiki, barani Asia katika nchi kama India na China, linalimwa kwa wingi nchini Jamaica, Ameriki ya Kati, na nchini Tanzania linalimwa zaidi katika mikoa ya Kigoma, Tanga, Morogoro, Pwani, Mbeya na Kilimanjaro.

Tangawizi inatumika kama kiungo katika kuongeza ladha, harufu na kuchangamsha katika vinywaji (kama soda, juisi, vilevi n.k) na vyakula mbalimbali kama mikate, biskuti, keki na nyama za kusaga.

Pia, inatumika katika viwanda vinavyotengeneza dawa ya tiba mbalimbali, kama dawa za meno, kikohozi, tumbo na muwasho wa ngozi.

Zao hilo linastawi katika maeneo yenye hali ya kitropiki, kutoka usawa wa bahari hadi mwinuko wa mita 1,500 au zaidi, ikihitaji mvua kiasi cha milimita ,1200 hadi 1,800 na joto la wastani wa nyuzi za sentigredi 20 hadi 25, hapo ustawi bora unashuhudiwa kwenye udongo tifutifu, wenye rutuba na usiotuamisha maji.

**SHAMBANI SAME**

Mkoa wa Kilimanjaro, zao hilo hulimwa wilayani Same na kwa takribani miaka 30 sasa bado wanakabiliwa na matatizo ya miundombinu.

Nipashe ikiwa katika Kata ya Miamba, umbali wa kilomita zaidi ya 95 kutoka stendi kuu ya mabasi yaendayo mikoani, mjini Moshi inakutana na wakulima, akiwemo Godson Mzava.

Anasema, huwa analima zao hilo milimani akitumia umwagiliaji kupitia miundominu ya kujitengenezea, akisema ni hali inayosababisha uharibifu wa vyanzo vya maji, kutokana na baadhi ya wenye fedha kutumia fursa hiyo kupeleka mipira karibu na vyanzo hivyo.

Mzava anafafanua kwamba, bado wanakabiliwa na tatizo la jiografia katika maeneo wanakolima tangawizi, akifafanua.

"Kila mkulima kwa kutumia ujuzi wake, hufanya jitihada za kutafuta maji kwenye mito na mifereji mbalimbali ya asili, hivyo wenye pesa zaidi ndio wana uwezo wa kununua mipira mingi zaidi na kuchukua maji kutoka kwenye umbali mrefu. Hii inatunyima haki sisi wakulima wengine."

Mkulima mwingine, Hawa Ramadhani, anasema kilimo hicho kinategemea nguvu na uwezo wa mkulima kujitafutia maji kwenye vyanzo, pia analalamikia usimamizi duni wa mamlaka za maji.

"Tupo wakulima wengi sana tunaolima tangawizi hapa Same, ila hatuna miundombinu inayoeleweka, hali ambayo kila mkulima huwahi kwenye chanzo na kuchukua maji hali inayopelekea uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji, hasa nyakati za kiangazi," anasema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wakulima wa Tangawizi Kata ya Mamba Miamba, Growers Assosiation, Mbaraka Ally, anasema kwa sasa wakulima wanalima kwa kutengeneza miundombinu wenyewe.

Katika hilo, anaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kujenga bwawa, pamoja na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji wilayani humo.

Anafafanua: " Wakulima wapo zaidi ya 3000 kwa upande wa milimani ambao hulima Kilimo cha Umwagiliaji na tunazalisha zaidi ya tani 25000 kwa mwaka na ikiwa tutasaidiwa kupata miundombinu bora, ikiwa ni pamoja na mabwawa yataweza kutusaidia kupata maji kwa kiwango kikubwa."

**MBUNGE KILANGO**

Mbunge wa Same Mashariki, Anne Kilango, anasema jimboni kwake, kuna tarafa mbili, zote zinalima tangawizi, wapo wanaolima kiwango kikubwa na baadhi kidogo.

Anasema, wananchi hao wamelima tangawizi kwa zaidi ya miaka 30 katika miundombinu isiyoridhisha, akiomba iboreshwe ili kuwasaidia kuzalisha kwa tija.

"Tatizo langu ambalo nalilia serikali ni miundombinu ya umwagiliaji iboreshwe ili waweze kulima kwa ukubwa zaidi," anasema mbunge

Anaitaka serikali ikae pamoja na wakulima kuona namna inaweza kuboresha miundombinu hiyo, kuendana na jiografia ya maeneo hayo,

Anafafanua, kwa sasa serikali imefika hapo kusoma mazingira kupitia wataalamu wake, ili ione namna itakavyoweka miundombinu ya kudumu, kwa kutenga bajeti zake kupitia Wizara ya Kilimo.

**MTAALAMU UMWAGILIAJI**

Mhandisi Raymond Mndolwa, ni Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Umwagiliaji, akiwa wilayani Same anasema amekuwa hapo kutathimini miundombinu ya umwagiliaji wa tangawizi ulivyo.

"Uwekezaji wa tume tunaweza kuufanya baada ya kujua mahitaji , lazima tujifunze(study) , licha ya kuwa tume imekuwa ikifanya kazi na ninyi ila kidogo kidogo, kwa kuboresha mifereji, lakini kwa sasa tumekuja tuweze kuangalia namna ya kufanya uwekezaji mkubwa wenye matokeo chanya," anaeleza.

Anasema, uwekezaji huo utakuwa mkubwa na utakaodumu, ili kusiwepo uwekezaji wa kujirudia kila wakati, kutokana na fedha inayotolewa na serikali siyo nyingi.

"Niliambiwa mifereji tisa ambayo ndio mwanzo tume ya umwagiliaji ilikuwa ikiifanyia kazi, lakini kauli yako (Mbunge Kilango) uliyoizungumza hapa, inaonyesha ni wakulima wote wa tarafa zote mbili wahudumiwe," anasema.

Anaendelea: "Sasa kwa ufinyu wa bajeti tuliyo nayo, mimi niombe unikubalie tuanze na ile mifereji tuliyokuwa tunaifanyia kazi. Pamoja na ufinyu wa bajeti yetu na haikuwa ndani ya bajeti yetu, nikuahidi mheshimiwa mbunge kuwa ile mifereji tisa tutaifanyia kazi.

"Tunataka kuboresha kilimo cha tangawizi kiwe cha ufanisi zaidi, lakini pale tunapokuja kuboresha, wakulima tunaomba muwe mstari wa mbele katika kulinda kile kitakachoboreshwa."

Rai yake anataka usimamizi wa kiuongozi, kwamba wawasimamie watendaji watakaofika, kufanya kwa ubora unaotakiwa, kwa sababu miradi mingi inafanyika na kufa muda mfupi, kutokana na kasoro ya kukosekana uaminifu.

Hapo anatoa mfano, kuwapo skimu za umwagiliaji mashambani zilizojengwa zama za uongozi wa nchi awamu ya kwanza, bado zinatumika kwa ubora wa hali ya juu, ilhali za baadaye sasa zimekosa viwango.

"Tutajenga miundombinu na kuisimamia katika kuhakikisha inalindwa, ikiwa na matatizo tume itakuja kutekeleza, ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho madogo na makubwa, ili wakulima walime kwa tija zaidi.

"Hivyo, hamasisheni na wenzenu ambao bado hawajalipa tozo kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni na mwaka wa pili, tutaweza kubuni," anashauri.



Sehemu ya mabomba yanayosafirisha maji kutoka kwenye chanzo, kwenda kwenye baadhi ya mashamba ya tangawizi yaliyopo milimani.

# Samia mgeni rasmi Siku ya Mashujaa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Mashujaa ambayo kitaifa yatafanyika Julai 25, mwaka huu, jijini hapa.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukagua maandalizi ya maadhimisho hayo.

"Mwaka huu mkoa wetu umepewa heshima ya kuwa mwenyeji kwani ipo mikoa mingi nchini ambayo inavyo viwanja kama hivi vya mashujaa. Nitoe wito kwa wananchi wa Dodoma pamoja na mikoa jirani kujitokeza kwa wingi siku hiyo ya maadhimisho ambayo mgeni rasmi atakuwa mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.



Aliipongeza Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi kwa namna ambavyo imekamilisha maandalizi ya maadhimisho hayo kwa asilimia kubwa.

"Lengo la kuja hapa sisi kama viongozi wa mkoa huu mwenyeji ni kuona namna gani maandalizi yanaendelea. Niwapongeze kwa hatua mliyofikia hadi sasa ni hatua nzuri sana.

Mambo yaliyobaki tunatumaini mtayakamilisha ndani ya wakati ili kufanikisha tukio hili," alisema.

Mtaka alisema pamoja na sherehe za maadhimisho hayo, pia kutakuwapo na matukio mbalimbali kabla na baada ya hapo.

"Kabla ya maadhimisho haya, Julai 24 saa 6:00 usiku mimi pamoja na viongozi mbalimbali wa kitaifa tutafanya tukio la kuwasha mwenge ambao pia utazimwa saa 6:00 usiku wa Julai 25 na Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe," alisema Mtaka.

Hata hivyo, alisema uongozi wa mkoa huo utashirikiana na jiji pamoja na kamati ya maadhimisho ya taifa kuangalia namna ya kulifanya eneo hilo kuwa endelevu kwa kuanzisha shughuli mbalimbali.

Mkurugenzi wa Maadhimisho ya Taifa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Batholomeo Jungu, alisema maandalizi ya tukio hilo yanaendelea vizuri na wanatarajia ifikapo Julai 25, kila kitu kitakuwa kimekamilika.

## Serikali sasa kujenga makumbusho ya marais

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI inakusudia kuanza ujenzi wa makumbusho ya marais jijini Dodoma ambayo yatakuwa na lengo la kuonyesha kwa jamii mchango na kazi zilizofanywa na viongozi hao.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Dk. Chana alisema makumbusho hayo yatatumika itatumika kuweka kazi na kumbukumbu za Marais wa nchi ili kuonesha mchango wao kwenye nyanja za kisiasa na kiuchumi kwa kipindi walichokuwa madarakani.

Aidha, alisema Wizara itaboresha mifumo ya Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari (TEHAMA) katika Shirika la Makumbusho ya Taifa yaliyoko Dar es Salaam.

Kadhalika, alisema uboreshaji huo utasaidia kuhifadhi vizuri kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho pamoja na kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali hizo.

Pia alisema uimarishaji huo wa TEHAMA kwenye makumbusho ya taifa utasaidia serikali kukusanya mapato zaidi ya kuwahudumia wananchi wake.

Kadhalika, alisema wizara itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa maliasili na malikale kwa kuboresha matumizi ya sayansi na teknolojia kwa kununua vifaa vya kisasa vya mawasiliano.

Dk. Chana alisema lengo la vifaa hivyo ni kuwezesha operesheni za doria kufanyika kwa tija na ufanisi zaidi pamoja na kuendelea na jitihada za kutangaza maeneo hayo ya malikale kuwa urithi wa taifa.

"Wizara itashirikisha jamii kutambua umuhimu wa kuhifadhi, kulinda na kuendeleza rasilimali hiyo ya malikale ili kunufaika na urithi huo," alisema.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli (kushoto), akizungumza na Balozi wa Brazil hapa nchini, Antonio Cezar, jijini Dodoma juzi, baada ya kusaini mkataba wa utekelezaji wa mradi wa zao la Pamba utakaotekelezwa katika wilaya za Magu, Misungwi na Kwimba. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

## Tanzania na Brazil kuleta mapinduzi kilimo cha pamba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TANZANIA na Brazil, zimeingia wameingia makubaliano ya kuleta mapinduzi ya kilimo cha pamba huku zaidi ya Sh. bilioni 2.1 zikitarajiwa kutumika katika mpango huo.

Mradi huo wa mwaka mmoja na nusu utatekelezwa kwenye mkoa wa Mwanza katika wilaya za Magu, Misungwi na Kwimba ambazo hulima kwa wingi zao hilo.

Akizungumza juzi kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, wakati wa kutia saini mkataba wa mradi huo, Mkurugenzi Msaidizi wa Sera, Gungu Mibavu, alisema unalenga kukuza zao hilo na kuongeza thamani ili kuwa na kilimo cha mazao mseto.

Mibavu alisema mradi huo unatarajia kuzifikia kaya 8,400 za wakulima wa Pamba ambazo zitanufaika katika mradi huo.

Alisema katika idadi hiyo asilimia 50 ya vijana, asilimia 30 wanawake na wanaume ni asilimia 20.

"Tunaishukuru sana serikali ya Brazil, Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kwa kuleta mradi huo hapa nchini. Tunaamini wakulima wa zao hilo pamoja na wadau wa kilimo hicho, watanufaika na utekelezaji wa mradi huo mkoani Mwanza," alisema.

Mibavu alisema mradi huo umejikita katika kuimarisha utafiti, usalama wa chakula pamoja na masuala ya lishe lakini pia utaongeza thamani ya mazao mengine.

Alisema hatua hiyo itasaidia mkakati wao wa ajenda ya 2030 ambapo wamepanga ifikapo mwaka huo kilimo kikue kwa asilimia 10.

Naye Mkurugenzi Mkazi wa WFP nchini, Brian Bogart, alisema mradi huo utaimarisha suala la chakula pamoja na kuwanufaisha wakulima.

"Naamini huu mradi utaleta mafanikio makubwa sana kwa taifa pamoja na wakulima katika maeneo ambayo unakwenda kutekelezwa," alisema Bogart.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba Tanzania, Marko Mtunga, aliishukuru serikali kwa kutia saini mkataba huo ambao utasaidia upatikanaji wa mbegu bora ambazozitaleta tija kwa wakulima na wananchi.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Geofrey Mkamilo, alisema kupitia mradi huo wataangalia kwenye maeneo ya utafiti wa mbegu inayokinzana na magonjwa kutokana na mbegu zilizopo ikiwamo UKM08 zinakabiliwa na magonjwa.

Balozi wa Brazil hapa nchini, Antonio Cesar, aliwataka kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kikamilifu kwenye maeneo hayo.



# Wakulima walipa kisogo zao la chai

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wakulima wa chai katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Iringa wameanza kuachana na kilimo cha zao hilo kwa kuanzisha kilimo cha parachichi kutokana na bei kutoongezeka kwa zaidi ya miaka minne mfululizo.

Wakizungumza jana kwenye kikao cha tathimini ya kilimo cha chai kilichofanyika jijini Mbeya, wadau na wakulima wa chai katika mikoa hiyo walisema uamuzi wa kuachana na kilimo hicho ni kutokana na gharama za uendeshaji kupanda huku bei ikibakia ile ile kwa muda mrefu.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, alisema bei ya majani mabichi ya chai haijapanda kwa muda mrefu hali ambayo inasababisha wakulima wengi kuona kuwa zao hilo haliwezi kuwakomboa kimaisha.

"Wakulima wanahoji kwa nini waendelee kulima chai wakati hawaoni faida yake. Wanasema gharama za uendeshaji zimekuwa kubwa, hivyo kuwasababishia hasara huku bei ikiwa ile ile kwa miaka minne mfululizo," alisema Dk Anney.

Alisema kwa sasa wakulima wengi wanabadilisha mashamba yao ya chai kwa kung'oa michai na kupanda parachichi zao ambalo bei kwa sasa imechangamka.

"Badala ya kuendelea kulima chai, kwa sasa wakulima wengi wanabadilisha mashamba yao kuwa ya parachichi kutokana na ukweli kwamba bei ya parachichi imekuwa nzuri ikilinganishwa na chai," alisema.

Naye Issa Mwaijumba ambaye ni mkulima wa chai mkoani Njombe, alisema bei ya chai haijapanda kwa miaka minne huku mbolea na dawa za kuulia wadudu zikizidi kupanda bei.

"Wakulima wengi tumeanza kukata tamaa kulima chai kwa sababu tukienda kununua mbolea tunakuta inauzwa kwa bei ya ghali lakini tunavuna na kuuza chai bei haiongezeki. Kwa kifupi kulima chai kwa sasa ni hasara tu," alisema Mwaijumba.

Kutokana na wakulima wengi kuanza kuachana na kilimo cha chai, Mradi wa IDH ulio chini ya Programu ya Agri Connect, umejikita katika uboreshaji wa zao hilo chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya.

Mradi huo umejikita katika kutoa elimu kwa wakulima namna ya kuzalisha chai yenye ubora jambo ambalo litasaidia kuongezeka kwa bei ya chai ya Tanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania, Dk. Emmanuel Simbua, alisema bei ndogo ya chai inasababishwa na ubora duni wa chai ya Tanzania ambao unatokana na wakulima wengi kuwa na miche ya miaka mingi.

Alisema kutokana na mashamba mengi ya chai nchini kuwa ya muda mrefu, si rahisi kushindanisha ubora wa chai na nchi ambazo zimeanza kulima zao hilo,kama vile Rwanda.

"Suluhisho la upatikanaji wa bei bora ya chai ni wakulima kung'oa miche ya michai ya zamani na kupanda mingine ili kuzalisha chai bora, tukiendelea kuvuna chai kwenye miche ya zamani hatuwezi kupambana na nchi zinazoingia kwenye tasnia hii kama vile Rwanda ambao miche ya chai yao ni mipya na inazalisha chai bora zaidi yetu," alisema Dk. Simbua.



Mbunge wa Jimbo la Lupa, wilayani Chunya, mkoani Mbeya, Masache Kasaka, akifungua pazia kuzindua zahanati ya kijiji cha Godima, Kata ya Chokaa juzi, iliyojengwa kwa ushirikiano wa wananchi na serikali kwa gharama ya zaidi ya Sh. Milioni 100. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mbunge kuhamasisha sensa wenye ulemavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya (CCM), Suma Fyandomo, amesema anatarajia kuanza kampeni ya kuhamasisha jamii kuwafichua watoto wenye ulemavu ili wahesabiwe wakati wa sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

Aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mchango wake kwenye suala hilo ambapo alisema wanashiriki kwa njia tofauti ikiwemo kutoa elimu kwa wananchi.

Katika mkoa wa Mbeya, alisema kuna kundi kubwa la watoto wenye ulemavu ambao wamekosa fursa ya elimu hasa katika Wilaya ya Rungwe kutokana na wazazi na walezi kuwaficha majumbani.

Alisema ili watoto hao wasisahaulike wakati wa sensa ni lazima elimu itolewe kwa wazazi, walezi na jamii nzima kuhusu umuhimu wa kundi hilo kufichuliwa na kuhesabiwa wakati wa sensa.

"Hili tatizo la watoto wenye ulemavu kufichwa lipo. Nimepokea taarifa ya watoto zaidi ya 100 wamefichwa majumbani na kwa sasa nimeanza hatua za awali za ufuatiliaji na kubaini maeneo ya vijiji husika "alisema Fyandomo.

Alisema akiwa mwakilishi wa wananchi, ni lazima alifanyie kazi pamoja na kuanza kampeni ya kutoa elimu, katika kata na vijiji pamoja na kutumia vipindi vya redio ili jamii ijue umuhimu wa zoezi la Sensa ya watu na makazi kwa watu wenye ulemavu.

"Nitakutana na maofisa ustawi wa jamii wa wilaya zote za mkoa wa Mbeya ili nipate taarifa ya takwimu za watoto waliotambulika ,na kuanza ufuatiliaji kwa maeneo ambayo nina taarifa nayo ili kuwaibua na kuwawezesha kupata haki za msingi hususan elimu, afya na malezi bora," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa wa Mbeya, Aika Temu, alisema serikali imewekeza kwenye shule za watoto wa kundi maalum ya Katumba Two iliyoko kata ya Ibigi wilaya ya Rungwe lakini tatizo lililopo ni wazazi kutokuwa na utayari wa kuwaficha huku fursa hiyo ikitumiwa na wazazi kutoka mikoa mingine ambao wana mwamko wa elimu kwa makundi maalumu.

"Shule ya Katumba Two ni maalum kwa makundi maalum wakiwepo walemavu kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, hivyo niwatoe hofu wazazi wawafichue ili waweze kutambulika na kuhesabiwa kwenye sensa Agosti 23," alisema.

## Wajikwamua na na tatizo la maji

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

ZAIDI ya Kaya 9,780 katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa, Mbarali mkoani Mbeya, zimeondokana na kero ya upatikanaji wa maji safi na salama baada ya mradi wa maji katika mji huo kukamilika.

Wananchi hao kwa muda mrefu walikuwa wanahangaika kupata huduma hiyo na kulazimika kutumia maji ya kwenye mifereji ya skimu za umwagiliaji hali ambayo inaelezwa kuwa ilikuwa inawasababishia magonjwa.

Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira (Ruwasa) Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Simon Bukuku, alikabidhi mradi huo juzi kwa wananchi baada ya kukamilika kwa asilimia 100 na kufanyiwa majaribio.

Alisema mradi huo umegharimu Sh. Milioni 372.2 fedha ambazo zimetolewa na serikali kuu na kwamba kwa sasa utakuwa unasimamiwa na jumuiya za watumia maji.

"Mradi huu umesuasua kwa kipindi cha mwaka mmoja baada ya mkandarasi aliyepewa zabuni kushindwa kusimamia vyema na Wizara ya Maji kurejesha miradi yote kwa mamlaka za maji kukamilisha ili wananchi wapate huduma ya maji safi na salama," alisema Bukuku.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji ya Mji wa Rujewa, Mhandisi Lestus Linda, alisema kukamilika kwa mradi huo kumeondoa adha kwa wananchi wa Mji huo ambao walikuwa wanapata shida ya kupata huduma hiyo jirani na makazi yao.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune aliwataka watendaji wa Mamlaka ya Maji Rujewa kutoa tenda za miradi kwa wakandarasi wasiotambua majukumu yao ili iweze kukamilika kwa wakati na jamii iondokane na adha ya maji kwa kutambua Serikali inawekeza fedha nyingi za miradi.



## Demokrasia Makini yajitosa kuhamasisha wananchi sensa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

HALMASHAURI Kuu ya Chama cha Demokrasia Makini Zanzibar imekutuna katika kikao cha kawaida kilichokuwa na ajenda ya kuhamasisha sensa ya watu na makazi.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar baada ya kikao hicho, Katibu Mkuu wa Chama hicho, Ameir Hassan Ameir, alisema jana mjini hapo kuwa lengo la kukutana kwao ni kuwataka wajumbe kuhamasisha wananchi kushiriki sensa kwa kukubali kuhesabiwa.

Alisema chama kimewataka wajumbe hao kila mmoja kwa nafasi yake kuhakikisha anahamasisha wananchi na wanachama wao kukubali kuhesabiwa ifikapo Agosti 23 kwa kuwa sensa ina manufaa makubwa.

"Ni wajibu wetu sisi wajumbe kuhamasisha wananchi na wanachama, tuwaambie umuhimu wa sensa katika nchi, kufanya hivyo kutasaidia wananchi kujitokeza kwa wingi siku hiyo," alisema.

Alisema kuwa sensa ya watu na makazi ina umuhimu mkubwa kwa taifa lolote duniani na serikali inapata kujua idadi ya watu wake, ikiwa ni sehemu ya kupanga mipango yake ya maendeleo.

Alisema kuwa chama chake kimeamua kuwahamasisha wajumbe na wanachama wake kujitokeza katika sensa, akisisitiza kuwa haina uhusiano na chama chochote na kila mmoja ana wajibu wa kulitelekeza hilo kwa nafasi yake bila ya kujali itikadi ya vyama vyao.

"Haitakuwa jambo zuri hata kidogo kwa zoezi la sensa kunasibishwa na itikadi ya vyama au mnasaba wa dini, hivyo ninawaomba ninyi wajumbe muwe mstari wa mbele kwenda kwa wananchi na wanachama wetu kuwapa elimu na kuwahamisha wakubali kuhesabiwa," alisema.

Alisema kuwa ili serikali ipanga mipango yake kwa uhakika katika kuwaletea maendeleo wananchi wake, lazima ijue idadi ya wananchi wake ikiwa ni njia rahisi ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Sensa itasaidia kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi ikiwamo afya, elimu na miundombinu, mambo ambayo yatarahishwa pale serikali itakapojua idadi ya watu wake, lazima tuwe mstari wa mbele kuhamisha wanachama wetu," aliongeza.

Ameir aliwataka wananchi kutokubali kudanganywa na kupotoshwa juu ya sensa kwa kuwa serikali ina nia njema na zoezi hilo kwa ajili ya kupanga maendeleo yake.

Pia aliwataka watendaji wa sensa kuwa weledi na kutumia busara wakati wa kutekeleza zoezi hilo pamoja na kufanya kazi kwa uzalendo bila ya kuingiza itikadi ya vyama na dini, ili kuepusha mikwaruzano isiyo ya lazima na wananchi pale wanapotakiwa kutoa taarifa.

Aliwapongeza Rais Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuweka wazi taratibu zote za sensa kwa wananchi.

# Mwinyi aahidi usafiri wa uhakika visiwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewahikishia wananchi wa Kisiwa cha Tumbatu kujenga gati la kisasa ili kuwarahisishia kufanya shughuli zao za kijamii na kiuchumi kwa kutoka eneo moja kwenda lingine bila ya usumbufu.

Alitoa ahadi hiyo jana wakati wa ziara yake ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo katika kisiwa hicho kilichoko Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema gati linalotumika sasa kuwavusha wananchi kutoka katika kisiwa hicho kwenda kufanya harakati zao za kimaisha, haliridhishi hivyo ni vyema kujengewa gati litakaloendana na wakati.

Rais Mwinyi aliwahidi wananchi wa kisiwa hicho kuwajengea gati ili kutatua kero ya usafiri inayowakabili kwa sasa.

"Imefika wakati kuhakikisha tunajenga gati nzuri ili kuona wananchi wanafanya safari zao kwa uhakika na usalama wao," alisema.

Dk. Mwinyi alisema kutokana na ugumu wa mazingira yaliyopo katika kisiwa hicho, wakati umefika kuwa na hospitali kubwa ya wilaya ndani ya Tumbatu ambayo itaondoa usumbufu wa wakazi wa kisiwa hicho.

"Ninayo habari kwamba watu wa kisiwa hiki wanapoumwa, na hata wajawazito, lazima wasafirishwe kwenda upande wa pili na wakati mwingine vyombo vinakuwa havipo au hali ya hewa ya bahari inakuwa ya ngumu na watu wanapoteza maisha.

"Hivyo, serikali itajenga hospitali yenye hadhi ya wilaya inayofanya upasuaji ili huduma za afya zipatikane hukuhuku bila ya kuvuka maji," aliahidi.

Akizungumzia sekta ya maji, Rais Mwinyi alisema serikali imejenga tangi lenye ujazo wa lita milioni moja ili huduma hiyo ipatikane kwa ufanisi zaidi kisiwani humo.

"Ninazo taarifa kwamba maji Tumbatu yanatokea upande wa pili lakini yanasukumwa moja kwa moja, hakuna sehemu ya uhifadhi na pampu zikiharibika, watu hawana maji.

"Hivyo, tangi tulilojenga linakuja kuondosha changamoto hii kwa madhumuni ya kuhakikisha pale inapojitokeza hitilafu, basi yapo maji yaliyohifadhiwa na maji yasikosekane kwa kipindi kirefu," alibainisha.

Alikipongeza Chuo cha Mafunzo na mkandarasi aliyejenga tangi la maji kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kisiwa hicho na kuwaahidi watashirikiana katika kazi zingine alizoziahidi katika kisiwa hicho.

Alisema serikali ina mpango maalum ya kuwawezesha wavuvi na kuwapatia mikopo, hivyo aliwaomba kuchangamkia fursa hizo ili kujikwamua kiuchumi.

Mwakilishi wa Jimbo hilo, Haji Omar Kheir, alimshukuru Rais Mwinyi kupitia Wizara ya Elimu kwa kujenga madarasa ambayo yatasaidia wanafunzi wa msingi waliokuwa wanakabiliwa na msongamano mkubwa madarasani.

Katika ziara hiyo, Rais Mwinyi pia aligawa boti za uvuvi kwa wavuvi na wakulima wa mwani 35, benki ya CRDB ikitoka boti 129 kwa Unguja na Pemba zilizogharimu Sh. bilioni 1.8.



Baadhi ya mafundi wakiendelea na ujenzi wa tangi la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita milioni moja, katika Kisiwa cha Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Utendaji wa waziri wamkosha Rais

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amefurahishwa na utendaji kazi wa Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, ambaye anatoka katika chama cha upinzani cha ACT-Wazalendo katika kusimamia majukumu ya kazi katika wizara yake.

Amesema kuwa licha ya kutoka chama cha upinzani, waziri huyo anatekeleza vyema ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025.

Dk. Mwinyi alimtaja hadharanii waziri huyo wakati akifanya majumuisho ya ziara yake ya Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja katika ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakil Kikwajuni, Zanzibar juzi.

Alisema Waziri Mazrui ni hodari na mchapa kazi ambaye anaendana na kasi ya utendaji wake licha ya kwamba anatoka katika chama cha upinzani.

"Niseme wazi kuwa mawaziri wangu wote wanafanya vizuri, lakini Waziri Mazrui anafanya vizuri sana licha ya kwamba anatoka katika chama cha upinzani, anatekeleza vizuri sana ilani ya chama changu cha CCM," alisema.

Kauli hiyo ya Rais Dk. Mwinyi kuhusu Mazrui iliibua shangwe miongoni mwa waliohudhuria mkutano huo.

Akifafanua zaidi, Dk. Mwinyi alisema katika baraza lake la mawaziri lenye sura ya Umoja wa Kitaifa, wapo mawaziri wawili tu wanaotoka katika chama cha upinzani cha ACT-Wazalendo ambao ni Waziri Mazrui na Omar Said Shabani, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, kati ya mawaziri 16 wanaounda baraza hilo.

Alisema angekuwa na ushawishi, angemshawishi Waziri Mazrui kujiunga na CCM kutokana na kasi yake ya utendaji kazi katika uongozi.

Dk. Mwinyi alisema ameridhishwa na miradi ya ujenzi wa hospitali 11 za wilaya na mkoa zinazojengwa Unguja na Pemba kupitia fedha za kukabiliana na athari za UVIKO-19.

Alisema ujenzi wa hospitali hizo unaendelea vizuri na amefurahishwa na kasi na ubora wa ujenzi wa hospitali hizo ambao umezingatia viwango vya kisasa vyenye kulingana na mahitaji ya sasa ya makundi yote ikiwamo yenye mahitaji maalum.

"Matarajio yangu ujenzi wa hospitali hizi utakapomalizika, kwa kiasi kikubwa utasaidia na kupunguza msongamano wa wagonjwa ambapo hakuna sababu tena ya mgonjwa kuletwa mjini kwa sababu hospitali za kisasa zipo vijijini," alisema.

Mazrui ambaye ni mfanyabiashara, kitaaluma ni mhandisi katika masuala ya ujenzi, alikuwa waziri katika awamu ya sita chini ya Rais Dk. Ali Mohmed Shein katika serikali ya kwanza chini ya muundo wa Umoja wa Kitaifa, akiongoza Wizara ya Biashara na Viwanda.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA VYETI



**FARIJI RAPHAEL MWASILE** anatangaza kupotea kwa vyeti vya kidato cha nne chenye index namba : **S0956/040** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ILEMBO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2007 na cha kidato cha sita chenye index namba: **S0417/0706** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MWAKALELI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2010. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **DAR/STA/RB/288590/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANATH KOKUSIMA HASHIM** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo No. **IRDP-LZC/CRP/14/1519** kilichotolewa na Chuo cha **INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT PLANNING** mwaka 2015.Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MW/RB/11954/2018.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**JANUARY LUCAS NJOZI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA, YENYE NAMBA **TAE 285058** KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. **MOR/MOR/RB/289052/2022**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA, KANDA YA BUKOBA**
**RUFAA NA. 92/2021**

**YANAYOTOKANA NA KESI YA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MULEBA Na. 15/2016**

**MOHAMED AKIBARU KADURU (Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu Akibaru Mohamed Kaduru ......................MUOMBA RUFAA**

**DHIDI YA**

**1. SADAT MTEGAGURA ..........................1ST MJIBU RUFAA**
**2. AMINI AKIBARU ................................2ND MJIBU RUFAA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**Kwa AMINI AKIBARU Popote Ulipo**

Hii ni kukutaarifu kwamba shauri la rufaa ya madai tajwa juu imepangwa kusikilizwa tarehe 11 mwezi Agosti mwaka 2022 saa 3:00 asubuhi, mbele ya Mh. Jaji MWENDA wa Mahakama Kuu, Kanda ya Bukoba. Kwa hiyo unapaswa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria. Endapo hutohudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako shauri hili litasikilizwa bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo hii tarehe 18 mwezi Julai mwaka 2022.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
BUKOBA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**

**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**

**Shauri la Madai Na.74/2022**

**Jina la Mdai ......................BARNABAS MAAGI**

**Jina la Mdaiwa ............. EZEKIEL MPOLO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
***(Kanuni ya 18 ya kanuni ya taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)***

**KWA. EZEKIEL MPOLO**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA TSHS. 1,800,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 27 Mwezi 07 Mwaka 2022 saa 2:00 Asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20 Mwezi 07 Mwaka 2022

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KARANGAI NAIMANI AKYOO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BAJAJI BOXER** yenye namba za usajili **MC 228 ANK,** yeyote atakayeiokota ataoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa
**ARU/ARU/RB/287625/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZINAT ARIF SULEMAN**
ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya gari **TOYOTA (MARK II)** yenye namba za usajili **T 897 DBQ.**
Chasis namba: **GX1106022079**
Engine Namba: **1G5825120.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo Cha Polisi.
Taarifa ya Polisi RB namba **IRI/IRI/RB/288531/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya MAKOLE**

**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**

**Shauri la Madai/Ndoa Na 54/ 2022**

**Jina la Mdai TABIA JOSHUA LEUNA**

**Jina la Mdaiwa ALPHONCE SUMBILA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa ALPHONCE SUMBILA**
**DAR ES SALAAM**

Kwa kuwa Mdai ameleta **Madai YA TALAKA**
Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya tarehe **26/07/2022 saa 08:00** asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikiliza shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria sikuiliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20 Mwezi 07 Mwaka 2022

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya MOSHI MJINI kituo cha MOSHI mkoa wa KILIMANJARO usimamizi wa mirathi na 140/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ROSE JOSHUA MOLLEL WA KCMC KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA NEEMA JOSHUA MOLLEL**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu anaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 10 mwezi 08 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 21 mwezi 07 mwaka 2022

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Makole**
**Kituo cha Makole Mkoa Dodoma**

**Shauri la Madai Na.241/2021**

**Jina la Mdai ......................VICTOR SHIKUSIRIE**

**Jina la Mdaiwa ............. HEMED RAMADHANI LUKINDO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

***(Kanuni ya 18 ya kanuni ya taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)***

**KWA. HEMED RAMADHANI LUKINDO**
**DODOMA MAILI MBILI**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA TSHS. 12,000,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 01 Mwezi 08 Mwaka 2022 saa 8:00 Asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20 Mwezi 07 Mwaka 2022

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Jinsi joto kali linavyohangaisha Ulaya

## ● Watu washauriwa kutotoka ndani ● shule zafungwa, misitu yawaka moto

Na Maulid Mmbaga



Zimamoto Ureno wakiendelea na jitihada za kuukabili moto unaoteketeza msitu. **PICHA: BBC.**

BARA la Ulaya limeshuhudia ongezeko la joto kali lililovunja rekodi na kusababisha madhara mbalimbali ikiwamo watu kupoteza maisha, kusimama kwa shughuli za kiuchumi na misitu kuteketea kwa moto.

Nchi za Ufaransa, Uingereza, Ureno na Ujerumani joto lilivunja rekodi na kufikia nyuzijoto zaidi ya 40, jambo ambalo halikuwahi kutokea katika eneo hilo.

Kwa mujibu wa mamlaka ya Ureno zaidi ya watu 238, wamepoteza maisha kutokana na joto kali, huku wazima moto wakihangaika kuzima moto unaoteketeza hifadhi ya misitu inayotanda eneo la Mediterania.

Maelfu ya wataalamu wa zima moto wanaendelea kukabiliana na janga la moto katika nchi za Ureno, Hispania na Ufaransa, huku wimbi la joto kali likionyesha kutokuwa na dalili ya kupungua kwa haraka.

**WANANCHI WAFUNGUKA**

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu mmoja wa raia wa Tanzania anayeishi jiji la Birmingham nchini Uingereza, Florence Mugarula, alisema kutokana na hali hiyo mamlaka zimekuwa zikihimiza watu kunywa maji mengi na kama hakuna ulazima wa kutoka nje ni vyema kukaa ndani.

Alisema nikweli hali ya joto imekuwa iko juu katika majira ya kila mwaka, lakini kipindi hiki imevunja rekodi kwa kufikia nyuzi joto 40 kwa juma lililopita.

"Kwa namna moja au nyingine hali hii imeleta athari katika baadhi ya maeneo mfano maeneo mengi ya kazini pamekuwepo na kusimama kwa kazi kwa muda kadhaa ili wafanyakazi wapate nafasi ya kunywa maji, hii imezorotesha utendaji kazi kwa kiasi flani," alisema Mugarula.

Aliongeza kuwa siku ya Jumatano ya wiki hii shule nyingi zilitangazia wazazi wasipeleke watoto shule kutokana na walimu kushindwa kumudu kufundisha watoto madarasani kwa sababu ya joto.

Pia alisema kwa mazingira ya huko watoto wasipokwenda shuleni ina maana na mzazi pia hawezi kwenda kazini hivyo inabidi abaki kuangalia watoto nyumbani.

Kitendo hicho kimeathiri utendaji wa wazazi kazini na pia imevuruga ratiba ya shule kwa watoto.

Vile vile anasema hali hiyo kimsingi inaongeza gharama za maisha kwa kiasi fulani kwakuwa watu wanalazimika kuwasha viyoyozi ambavyo vinatumia zaidi umeme na gesi.

"Kwa upande wa kiafya watu wamekuwa na hali ngumu hasa wazee na watoto kutokana na kukaukiwa na maji mwilini kutokana na hali ya joto isiyokuwa ya kawaida," alisema na kuongeza "Hata hivyo mamlaka zimejitahidi sana kutoa tahadhari na kuhakikisha kila mtu anabaki salama kupitia matangazo mbalimbali katika vyombo vya habari, mbao za matangazo barabarani na makazini," anasema Mugarula.

Anasema hali hii imeleta mabadiliko katika kipindi cha siku tatu ambapo kiwango cha joto kimekuwa cha juu kupita kiasi.

Naye Athuman Mtulya, mtanzania anayesoma Chuo Kikuu cha Leeds kilichopo katika jiji la Leeds Kaskazini mwa Uingereza, anabainisha kuwa hali ya hewa ya juzi ilirudi kuwa ya kawaida.

"Toka jana (juzi) hali imerejea kuwa sawa, joto kali lilikuwa Jumatatu na Jumanne, hali hiyo iliathiri kwa kiasi kikubwa, baadhi ya watu hawakwenda kazini na huduma za usafiri zilisitishwa katika baadhi ya maeneo," anasema Mtulya.

Alisema hali ya joto kupita kiasi katika maeneo hayo pia ilikuwa na athari za kiuchumi na katika pato la watu hususani wanaofanya kazi za vibarua na wafanyabiashara za huduma za moja kwa moja kwa watu.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya kuaminika, Kaskazini mwa Ureno, rubani alifariki wakati ndege yake ya kusaidia shughuli za zima moto ilipoanguka katika eneo la Foz Coa, karibu na mpaka wa Hispania.

Pia kwa mujibu wa BBC, moto uliosababishwa na hali ya joto kuwa kubwa uliteketeza maeneo ya kusini magharibi mwa mkoa wa Gironde nchini Ufaransa, ambapo zaidi ya watu 12,000 wamehamishwa katika makazi yao.

Inaelezwa kuwa vipindi vya joto vimekuwa vikitokea mara kwa mara, lakini mwaka huu wimbi kali zaidi la joto limeshuhudiwa kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi inayosababishwa na uharibifu wa mazingira.

Mamlaka ya hali ya hewa Ufaransa imetabiri viwango vya joto vya hadi nyuzi joto 41 katika sehemu za kusini mwa nchi huku rekodi mpya za joto zikitabiriwa kuendelea.

Waziri wa Mambo ya Ndani Gerald Darmanin alisema moto hadi sasa umeteketeza hekta 10,000 ambazo ni sawa na ekari 25,000 za ardhi, huku akisifu jitihada za wazima moto zinazoendelea kukabili tatizo hilo.

"Kila kitu kilikwenda kwa haraka sana, moto pia ulikuwa mkubwa," anasema Darmanin.

Moto mkubwa mwingine umeteketeza kaskazini mashariki mwa jiji la Porto nchini Ureno na kuharibu hekta 30,000 sawa na ekari 75,000 za ardhi.

Sehemu zingine za Bahari ya Mediterania zimeathiriwa ikiwemo Italia, huku serikali ikitangaza hali ya hatari katika Bonde la Po lililoharibiwa ambalo ni mto mrefu zaidi nchini humo.



Wananchi wakipooza miili kutokana na joto kali Madrid Hispania. **PICHA: DW.**

# KMC YAJIPANGA KUFUMUA KIKOSI, BIGIRIMANA ANUKIA

**Na Saada Akida**

KATIKA kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana amesema anahitaji kusajili wachezaji wapya wanne na katika rada zao yupo mshambuliaji wa Namungo, Blaise Bigirimana, imefahamika.

Hitimana aliliambia gazeti hili jana nafasi anazohitaji kuboresha ni pamoja na beki wa kati, kiungo na washambuliaji ili kuhimili ushindani unaotarajiwa kuongezeka.

Kocha huyo alisema atafanya usajili wake kwa kuzingatia mapungufu aliyoyabaini katika kikosi chake lakini akiitaja nafasi ya ulinzi ndio iliwasumbua zaidi.

Alisema wanafanya usajili katika nafasi zote kwa sababu ya wachezaji wengi wamemaliza mikataba na baadhi kupata nafasi ya kwenda kujaribu changamoto kwa timu zingine.

"Tutasajili kwa kuzingatia mapungufu tuliyokuwa nayo katika msimu uliopita, nakiri nahitaji zaidi beki wa kati, na huenda tukafanya usajili katika nafasi zote kwa sababu baadhi ya wachezaji wameamua kwenda kusaka timu mpya," alisema Hitimana.

Aliongeza watajipanga imara kwa sababu wanafahamu ushindani katika Ligi Kuu msimu ujao utaongezeka kwa sababu timu zote zimejiimarisha na zinataka kufanya vizuri.

"Ni kweli msimu uliopita tulicheza mechi zetu kwa presha kubwa kwa sababu tulikuwa na madhaifu katika kikosi chetu, sasa tumeanza kufanyia kazi ikiwamo kusajili nafasi ambazo zina changamoto," alisema Hitimana.

Kuhusu usajili wa Bigirimana, alisema ana nafasi kubwa ya kutua katika kikosi chake endapo watafikia makubaliano kutokana na kuhitaji maboresho katika safu ya ushambuliaji.

"Bado sijakutana na viongozi kuona usajili ambao wamefanya, sina uhakika wa moja kwa moja, kuhusu Bigirimana, inawezekana tumeshamnasa kwa sababu ya ripoti yangu imeelekeza tunahitaji mshambuliaji," alisema kocha huyo.

Aliongeza amesharejea nchini na anatarajia kukutana na mabosi wa timu hiyo ili kuandaa mipango ya timu yake kuingia kambini wiki ijayo ili kuanza maandalizi ya msimu mpya.

Katika hatua nyingine KMC imetangaza kuachana na baadhi ya wachezaji wake ambao ni Hassan Kessy, Dennis Richard, Sudi Dondola, Ally Ramadhani na Dickson Kibabage.



Beki wa kushoto wa Timu ya Soka Taifa (Taifa Stars), Dickson Kibabage (kulia), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Sudan Kusini katika mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa JK Park jijini Dar es Salaam. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba Queens yatarajia makubwa

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Simba Queens umesema kikosi chao kimeimarika na wako tayari kwenda kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika kuanzia Agosti 13 hadi 27, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Asha Baraka alisema msimu huu wamejipanga kikamilifu kwa ajili ya kutwaa ubingwa wa michuano hiyo kwa kusajili wachezaji wenye uzoefu na mashindano ya kimataifa.

"Mwaka jana tuliiwakilisha nchi kule Kenya, lakini tulikuwa na mapungufu kidogo kwa sababu ilikuwa ni mara yetu ya kwanza, lakini safari hii tumejifunza michuano hii inataka nini na wachezaji wa aina gani, ndiyo maana unaona safari hii tumefanya usajili wa nguvu, tunaamini tutafanya vizuri," alisema Mjumbe huyo.

Aliwataja baadhi ya wachezaji waliowasajili ni Philomena Abakah kutoka Berry Ladies ya Ghana, Ibinabo Alex (Confiuennce ya Nigeria), Aquino Corazone (Gaspo Youth ya Kenya) na Topistar Situma kutoka Vihiga Queens ya Kenya.

Simba Queens iimepangwa Kundi B ikiwa pamoja na GRFC ya Burundi, Yei Joint Stars (Sudan Kusini) na SHE Corporate WFC ya Uganda.

Kundi A linaundwa na CBE ya Ethiopia, AS Kigali (Rwanda), Warriors Queens (Zanzibar) na FOFILA PF ya Burundi. Mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Vihiga Queens haitashiriki msimu huu kutokana na Kenya kufungiwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

## Warriors Queens yaiwinda CECAFA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa mabingwa wa soka la wanawake Zanzibar, Warriors Queens, Abdallah Bakari amesema timu yake inaendelea kujiimarisha kuelekea mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati ambayo yatafanyika kuanzia Agosti 13 hadi 27, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa juzi nchini Morocco, Warriors Queens wamepangwa Kundi A pamoja na CBE kutoka Ethiopia, FOFILA PF (Burundi) na As Kigali ya Rwanda wakati Kundi B linaundwa na wenyeji Simba Queens ya Tanzania Bara, GRFC (Djibouti), She- Corporate WFC (Uganda) na Yei Joint Stars kutoka Sudani Kusini.

Bakari alisema anaamini michuano ya mwaka huu itakuwa migumu zaidi ukilinganishwa na msimu uliyopita kwa sababu timu zote zimejipanga kushindana.

"Tumejipanga kufanya vizuri, michuano hii sio rahisi kwa sababu kila timu inataka kushindana na kufanya vizuri, hivyo na sisi tunaendelea kujipanga ili tufanikiwe na kusonga mbele, hatutaki kuishia katika hatua ya makundi," alisema Bakari.

## Mwanza kuendeleza vipaji UMITASHUMTA

**Na Vitus Audax, MWANZA**

SERIKALI mkoani Mwanza imeahidi kuendeleza vipaji vya wanafunzi watakaoibuka kidedea katika michezo mbalimbali ya shule za msingi maarufu UMITASHUMITA ngazi ya taifa mwaka huu ambayo itafanyika mkoani Tabora.

Akizindua mashindano hayo katika ngazi ya mkoa juzi, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, aliwataka wanafunzi hao kutoka wilaya saba kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo yote kwenye ngazi ya taifa.

Gabriel aliwataka vijana hao kuonyesha juhudi, nidhamu na ushindani mkubwa ili kuiwakilisha vyema Mwanza watapokuwa katika mashindano hayo.

"Kwa sasa tunajiandaa tu kuwapokea mkitoka katika mashindao haya kitaifa, pia niwaahidi mwaka huu tutawapokea na zawadi kubwa endapo mtakuja na ushindi katika michezo yote," alisema mkuu huyo wa mkoa.

Ofisa Elimu ya Msingi Mkoa wa Mwanza, Martin Nkwabi, aliahidi kurejea na ushindi kutokana na wanafunzi hao kunolewa vizuri na baadhi ya makocha wa soka wa timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania bara.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DE JONG AICHAGUA BAYERN

MCHEZAJI anayelengwa na Manchester United, Frenkie de Jong hataki kuondoka Barcelona - lakini iwapo atahama, kiungo huyo wa kati wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 25, angependelea kujiunga na Bayern Munich au Chelsea. (***Sport***)

### KOUNDE SAFI CHELSEA

JULES Kounde anatazamiwa kufanyiwa vipimo vya afya na Chelsea ndani ya saa 48 zijazo baada ya The Blues hao kuafikiana na Sevilla kwa ada ya pauni milioni 55 kwa ajili ya kumnunua mlinzi huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 23. (***Sun***)

### GVARDIOL SOKONI EPL

CHELSEA pia wamemfanya mlinzi wa RB Leipzig mwenye umri wa miaka 20 kutoka Croatia, Josko Gvardiol kuwa mlengwa wao mkuu kuchukua nafasi ya beki wa pembeni wa Hispania, Cesar Azpilicueta (32), ambaye anatarajiwa kujiunga na Barcelona. (***Sun***)

### DENNIS KUTUA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Watford raia wa Nigeria, Emmanuel Dennis mwenye umri wa miaka 24, ambaye thamani yake inakadiriwa kuwa pauni milioni 25. (***Mail***)

### MONACO YAIGOMEA LEICESTER

KLABU ya Leicester imekataa dau la pauni milioni 15 kutoka kwa Monaco kwa ajili ya kumnunua, Boubakary Soumare, kwani wanataka kurejesha zaidi ya pauni milioni 23 walizotumia kumnunua kiungo huyo wa kati Mfaransa mwenye umri wa miaka 23. (Mail)

### UNITED YAMWOTA ANTONY

KLABU ya Manchester United bado inamtaka winga wa Ajax Mbrazil, Antony mwenye miaka 22, licha ya kwamba dau la pauni milioni 51 lilikataliwa. (***Talksport***)

### REGUILON ATAJWA BARCA

BARCELONA wamemtambua mchezaji wa Tottenham Hotspur, Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 25, kama beki mbadala wa kushoto anayelengwa kama hawatakubali makubaliano na Chelsea kumnunua Mhispania mwenzake, Marcos Alonso (31). (***Mundo Deportivo***)

### TAVARES ANUKIA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inafikiria kumnunua kwa mkopo beki wa kushoto wa Arsenal mwenye umri wa miaka 22, Nuno Tavares huku wakitafuta mbadala wa mlinzi anayelengwa na Manchester City, Marc Cucurella mwenye miaka 23. (***O Jogo***)

### HARRISON KUTUA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle imetoa ofa ya takriban pauni milioni 18 kumnunua winga wa Leeds United, Jack Harrison mwenye miaka 25. (***Football Insider***)

### LINGARD MAMBO SAFI

KLABU ya Nottingham Forest imempa mchezaji huru, Jesse Lingard mkataba wenye thamani ya pauni 200,000 kwa wiki huku wakipania kuwashinda West Ham katika vita kuinasa saini ya mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 29. . (***Mail***)

### MCNEIL AWEKWA SOKONI

KLABU ya West Ham na Crystal Palace wamewasiliana na Burnley kwa ajili ya kumnunua kiungo wao mwenye umri wa miaka 22, Dwight McNeil. (***Sky Sports***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL ASHANGAA UBORA WA WERNER

**Kocha afunguka mshambuliaji huyo ameshindwa kuonyesha...**

**LONDON,** ENGLAND

THOMAS Tuchel amesema haelewi kwa nini, Timo Werner hatakuwa na furaha Chelsea na amemtaka fowadi huyo "kuonyesha ubora" ili kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara.

Werner amevumilia miaka miwili ya kufadhaisha akiwa na The Blues hao kufuatia uhamisho wake wa fedha nyingi kutoka RB Leipzig misimu miwili iliyopita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani ameshindwa kujiimarisha katika kikosi cha kwanza, akiwa amefunga mabao 10 pekee katika Ligi Kuu England kwenye misimu miwili kwa klabu hiyo ya London.

Werner alifunga katika ushindi wa mabao 2-1 katika mchezo wa kirafiki dhidi ya Club America wikendi iliyopita na akapendekeza baada ya mechi hiyo anaweza kuondoka Stamford Bridge, kwani anahitaji kucheza kikosi cha kwanza kabla ya Kombe la Dunia nchini Qatar.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 alikosa kucheza kwa sababu ya jeraha la msuli wa paja wakati Chelsea ikichapwa mabao 5-3 kwa penalti na Charlotte FC siku ya Jumatano baada ya timu hizo mbili kumaliza mchezo kwa sare ya 1-1.

Tuchel aliibua sintofahamu juu ya matamshi ya Werner na kusema: "Ninashangaa, ningefurahi sana kama kijana mwenye mkataba katika klabu ya Chelsea niwe na furaha zaidi duniani."

Alipoulizwa jinsi Werner anavyoweza kuwa kwenye kikosi cha kwanza, Tuchel alijibu: "Onyesha ubora, chukua nafasi yako na utetee nafasi yako.

"Ningekuwa mmoja wa watu wenye furaha zaidi duniani kuwa na mkataba Chelsea."

Alipoulizwa kama atakuwa mchezaji wa Chelsea katika msimu ujao, Tuchel alisema: "Hakika, ni mchezaji wetu, hakika."

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,016,4
MECHI KALI
CRYSTAL PALACE
VERSUS
LEEDS
1 | 2.55
X | 3.54
2 | 2.35
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# FERNANDES: RONALDO ATABAKI MAN UNITED



**MANCHESTER, England**

BRUNO Fernandes amekiri hajui kama mchezaji mwenzake, Cristiano Ronaldo atabakia Manchester United msimu huu wa joto.

Ronaldo aliiomba United kuzingatia ofa za uhamisho kwa ajili yake mapema msimu huu wa joto, lakini bado hakuna uhamisho uliofikiwa.

Alipewa likizo na Mashetani Wekundu hao kwa sababu za kifamilia na hakujumuishwa kwenye kikosi chao cha maandalizi ya msimu mpya.

Kocha, Erik ten Hag tangu wakati huo amedokeza Ronaldo ataongeza muda wake wa kubakia katika klabu hiyo, ingawa Fernandes amefichua wachezaji wengine wa kikosi hicho bado wako gizani.

"Ni wazi tunapaswa kuheshimu uamuzi wa kila mtu," alisema.

"Sijui Cristiano alisema nini kwa klabu, kwa kocha, sijui nini kinaendelea ndani yake, lakini tunapaswa kuheshimu nafasi yake.

"Kutoka kwa kila kitu tunachojua, alikuwa na shida kadhaa za kifamilia, kwa hivyo lazima tuheshimu nafasi yake, tumpe nafasi na ndivyo hivyo.

"Cristiano alikuwa mfungaji bora wetu msimu uliopita, alituongezea mabao, lakini ni wazi si juu yangu, ni klabu ambayo inapaswa kufanya uamuzi na Cristiano anafanya chaguo lake mwenyewe.

"Kama nilivyosema, sijui kinachoendelea kichwani mwake, ikiwa anataka kuondoka, yote ni habari.

# Kounde anukia kusaini Chelsea

**LONDON, England**

CHELSEA wamepandisha ofa yao ili kufikia bei inayotakiwa na Sevilla ili kumnunua mlinzi, Jules Kounde, kwa mujibu wa 90min.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa analengwa kwa muda mrefu na Chelsea na wamerejea kwake baada ya kumkosa beki wa kati aliyepewa kipaumbele, Matthijs de Ligt, ambaye amejiunga na Bayern Munich akitokea Juventus.

Kama ilivyoripotiwa na 90min, The Blues walirejea katika meza ya mazungumzo kwa Kounde mapema wiki hii na kuwasilisha ofa yenye thamani ya euro milioni 55, lakini hiyo ilikuwa bado euro milioni 10 pungufu ya hesabu ya timu hiyo ya LaLiga.

Hata hivyo, Chelsea walisalia katika mazungumzo na sasa wameongeza euro milioni 65 ili kumnasa mchezaji huyo.

Na sasa Kounde ana nafasi kubwa zaidi kukamilisha uhamisho huo, ingawa maslahi kibinafsi yalikubaliwa mapema mwezi huu - na kuwapa Chelsea imani dili linaweza kuthibitishwa ndani ya siku chache.

Inaaminika kuwa Barcelona bado wanawasiliana na Sevilla, lakini bado hawajatoa ofa thabiti na Chelsea wana uhakika wa kukamilisha uhamisho wa mchezaji ambaye wamekuwa wakijaribu kumsajili kwa zaidi ya miezi 12.



## HABARI MICHEZO


28,582/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/07/22 | 19:15 | Kortrijk vs OH Leuven | 2.39 | 3.48 | 2.79 |
| 02. 23/07/22 | 21:30 | Hannover vs St. Pauli | 2.38 | 3.43 | 2.83 |
| 03. 23/07/22 | 21:30 | Sarmiento vs Colon Santa Fe | 2.42 | 3.14 | 3.14 |
| 04. 23/07/22 | 22:30 | Vila Nova GO vs Vasco da Gama | 2.63 | 2.73 | 3.08 |
| 05. 24/07/22 | 00:30 | Nautico PE vs Londrina PR | 2.30 | 2.97 | 3.36 |
| 06. 24/07/22 | 02:30 | CRB AL vs Novorizontino SP | 2.48 | 2.93 | 3.08 |
| 07. 24/07/22 | 02:30 | FC Cincinnati vs Nashville | 2.32 | 3.42 | 3.02 |
| 08. 24/07/22 | 02:30 | Orlando City vs Philadelphia Union | 2.37 | 3.43 | 2.93 |
| 09. 24/07/22 | 03:00 | Botafogo RJ vs Atletico Pr | 2.30 | 3.33 | 3.03 |
| 10. 24/07/22 | 03:00 | DC United vs Montreal Impact | 2.31 | 3.38 | 3.07 |
| 11. 24/07/22 | 03:30 | Sporting Kansas City vs Los Angeles FC | 2.90 | 3.50 | 2.35 |
| 12. 24/07/22 | 05:00 | Vancouver Whitecaps vs Chicago Fire | 2.28 | 3.45 | 3.05 |
| 13. 24/07/22 | 12:00 | Tokyo Verdy vs Yokohama | 2.90 | 3.30 | 2.42 |
| 14. 24/07/22 | 14:30 | Karlsruher SC vs Magdeburg | 2.50 | 3.40 | 2.70 |
| 15. 24/07/22 | 17:00 | Mechelen vs Royal Antwerp | 2.55 | 3.40 | 2.65 |
| 16. 24/07/22 | 22:00 | Westerlo vs Cercle Brugge | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 17. 24/07/22 | 22:00 | Juventude RS vs Ceara CE | 2.58 | 2.98 | 2.93 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 22/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:05 | 1858 | Crystal Palace vs Leeds | 2.60 | 3.58 | 2.29 |
| 16:00 | 3346 | Projek Fam-Msn vs Selangor Pkns | 5.10 | 3.92 | 1.54 |
| 18:00 | 3801 | Znicz Pruszkow vs Radunia Stezyca | 2.51 | 3.44 | 2.44 |
| 18:00 | 4402 | Komarno vs FK Pohronie | 2.20 | 3.55 | 2.90 |
| 18:00 | 4981 | Vilniaus Riteriai vs Dziugas | 1.50 | 3.88 | 5.69 |
| 18:30 | 5570 | PFC Spartak Varna vs Pirin Blagoevgrad | 2.09 | 3.24 | 3.19 |
| 18:30 | 5876 | FC KTP vs Japs | 1.46 | 4.33 | 5.51 |
| 19:00 | 1573 | Warta Poznan vs Wisla Plock | 2.29 | 3.04 | 2.99 |
| 19:00 | 2056 | Tallinna JK Legion vs Flora Tallinn | 13.70 | 6.85 | 1.14 |
| 19:00 | 3052 | First Vienna vs Blau Weiss Linz | 3.88 | 3.88 | 1.71 |
| 19:00 | 4482 | Skra Czestochowa vs Chojnice | 2.38 | 3.10 | 2.80 |
| 19:10 | 1638 | SV Horn vs Sturm Graz II | 2.22 | 3.58 | 2.70 |
| 19:10 | 1995 | Amstetten vs Kapfenberg | 1.59 | 4.02 | 4.51 |
| 19:10 | 3804 | Austria Vienna II vs FC Liefering | 3.29 | 3.63 | 1.92 |
| 19:10 | 4430 | Vorwarts Steyr vs Rapid Vienna II | 2.15 | 3.45 | 2.91 |
| 19:30 | 1824 | Arab Contractors vs Ghazl EL Mahallah | 2.39 | 2.72 | 3.47 |
| 19:30 | 2787 | SV Darmstadt vs Sandhausen | 1.76 | 3.75 | 4.10 |
| 19:30 | 4297 | Fortuna Dusseldorf vs Paderborn | 2.19 | 3.50 | 2.95 |
| 19:30 | 5273 | Ceramica Cleopatra vs Al Masry Club | 2.46 | 3.07 | 2.92 |
| 19:30 | 5454 | Vendsyssel FF vs Hillerod | 1.74 | 3.45 | 4.23 |
| 20:00 | 2449 | Spartak Myjava vs FC Petrzalka 1898 | 2.14 | 3.60 | 3.00 |
| 20:00 | 4074 | Osnabruck vs Duisburg | 1.63 | 3.95 | 4.70 |
| 20:00 | 4137 | Midtjylland vs Silkeborg | 1.80 | 3.76 | 3.96 |
| 20:00 | 4858 | Sonderjyske vs Fremad Amager | 1.46 | 4.21 | 5.67 |
| 20:00 | 5555 | Zenit St Petersburg vs Kryliya Sovetov | 1.37 | 4.78 | 6.97 |
| 20:30 | 3171 | CS Mioveni vs Farul Constanta | 3.09 | 3.04 | 2.34 |
| 20:30 | 5336 | Neuchatel Xamax vs FC Aarau | 3.82 | 3.87 | 1.72 |
| 21:00 | 1613 | Istra vs Vsnk Varazdin | 2.11 | 3.29 | 3.10 |
| 21:00 | 2845 | CSKA 1948 vs Ludogorets Razgrad | 3.52 | 3.42 | 1.91 |
| 21:15 | 1234 | FC Thun vs AC Bellinzona | 1.62 | 4.10 | 4.50 |
| 21:15 | 4913 | Lausanne-Sport vs FC Schaffhausen | 2.25 | 3.50 | 2.71 |
| 21:15 | 5163 | NK Radomlje vs NK Celje | 2.55 | 3.33 | 2.45 |
| 21:30 | 2259 | Resovia Rzeszow vs Wisla Krakow | 3.49 | 3.15 | 2.02 |
| 21:30 | 4224 | Zlate Moravce vs MFK Skalica | 1.70 | 3.58 | 4.32 |
| 21:30 | 4372 | RB Salzburg vs Austria Vienna | 1.27 | 5.30 | 8.24 |
| 21:30 | 5312 | Jagiellonia vs Widzew Lodz | 1.97 | 3.28 | 3.48 |
| 21:45 | 1479 | Dundalk FC vs Finn Harps | 1.38 | 4.32 | 7.07 |
| 21:45 | 1511 | Waterford Utd vs Longford Town | 1.36 | 4.63 | 6.70 |
| 21:45 | 2192 | UCD Dublin vs Shelbourne | 5.13 | 3.35 | 1.65 |
| 21:45 | 4053 | Athlone Town vs Galway United | 7.81 | 5.27 | 1.28 |
| 21:45 | 4664 | Standard Liege vs KAA Gent | 3.75 | 3.50 | 1.91 |
| 21:45 | 5632 | Cobh Ramblers vs Bray Wanderers | 2.98 | 3.43 | 2.11 |
| 21:45 | 5868 | Wexford Youths vs Cork City | 4.32 | 3.83 | 1.65 |
| 22:00 | 1735 | Enppi Club vs Farco FC | 2.26 | 2.91 | 3.46 |
| 22:00 | 1774 | Sweden W vs Belgium W | 1.29 | 4.89 | 8.22 |
| 22:00 | 3497 | Mitre SdE vs All Boys | 2.27 | 2.89 | 3.18 |
| 22:15 | 1689 | Kordrengir vs Thor Akureyri | 1.69 | 3.93 | 3.93 |
| 22:15 | 5071 | Njarovik vs Throttur Reykjavik | 1.60 | 4.22 | 4.22 |
| 22:15 | 5569 | Augnablik vs Ellidi | 2.45 | 4.11 | 2.23 |
| 23:00 | 2227 | Ayacucho vs Cesar Vallejo | 2.03 | 3.24 | 3.34 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# UJENZI UWANJA WA KISASA MWEMBEYANGA WAANZA

**Na Faustine Feliciane**

UJENZI wa uwanja wa kisasa katika eneo la Mwembeyanga, Temeke jijini Dar es Salaam umeanza, imeelezwa.

Uwanja huo utahusisha viwanja vya michezo mbalimbali ikiwamo soka, netiboli na kikapu.

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, alisema ujenzi wa uwanja huo utagharimu kiasi cha Sh. milioni 998.

Jokate alisema uwanja wa mpira wa miguu utakaojengwa katika mradi huo utakuwa ni wa nyasi halisi huku miundombinu mingine iliyobakia itafanya kisasa.

"Mradi huu ukikamilika utalifanya eneo hili maarufu la Mwembeyanga kuwa la kisasa zaidi kwa kuwa na miundombinu rafiki, nafahamu hapa pamekuwa pakitumika kwa michezo mbalimbali, matamasha na mikutano, kukamilika kwake kutapafanya wananchi wa maeneo haya kuwa na sehemu sahihi ya kufanya michezo na kupumzika," alisema Jokate.

Aliongeza mara baada ya kukamilika kwa uwanja huo, wananchi wataendelea kutumia bure kwa shughuli za michezo na za kijamii.

"Eneo hili sasa litakuwa chini ya halmashauri, lakini hakuna mwananchi atakayetozwa fedha kuja kucheza au kupumzika hapa, isipokuwa wale watakaokuwa wakikodisha kwa ajili ya matamasha ya kibiashara hao wataendelea kufanya hivyo kwa usimamizi wa manispaa," Jokate alisema.

Kiongozi huyo alisema mbali na ujenzi wa viwanja hivyo, pia wataboresha mazingira ya eneo hilo kwa kupanda miti maeneo yote yanayozunguka eneo hilo.

"Ipo miti zaidi ya 1,900 ambayo itapandwa katika maeneo mbalimbali ya halmashauri yetu, na baadhi ya maeneo hayo ni hapa kwenye viwanja vya michezo," aliongeza Jokate.

Msimamizi wa mradi huo kutoka Wakala wa Ujenzi wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) wa Manispaa ya Temeke, Injinia Paul Mhere alisema mradi huo utasimamiwa na Kampuni ya Group Six International na utakamilika ndani ya miezi miwili.

"Kazi kubwa kwenye uwanja wa mpira wa miguu ilikuwa ni kuweka 'levo' uwanja na kuupima katika vipimo vinavyokubalika kama viwanja vingine rasmi vya mpira, baada ya hapo ni kuotesha nyasi za kisasa na kujenga miundo mbinu yake kuzunguka uwanja, kazi imeshaanza na mpaka sasa ndani ya wiki mbili tumefika asilimia 25," alisema Mhere.



Wanariadha wa Timu ya Mkoa wa Dar es Salaam wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam ili kujiandaa na mashindano ya UMISETA yanayotarajiwa kufanyika mkoani Tabora mwezi ujao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Nyankumbu yafanyiwa ukarabati

**Na Adam Fungamwango**

UWANJA wa Shule ya Nyankumbu Girls umeanza kufanyiwa ukarabati ili kukidhi sifa na hatimaye kuendelea kutumiwa na Geita Gold FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ujenzi huo unafanyika kwa ushirikiano kati ya wamiliki wa uwanja huo pamoja na mabosi wa Geita Gold FC.

Meneja wa Uwanja, Michael Yujin alisema mchakato huo umeanza rasmi baada ya kupokea barua kutoka katika Bodi ya Ligi Kuu na lengo ni kumaliza changamoto zilizoainishwa ikiwamo kumwagia maji ili kuotesha nyasi.


"Baadhi ya juhudi tumeshaanza kuzifanya, tunaendelea kumwagia maji, ingawa mabomba hayatoshi, lakini jitihada zimefanywa kuwasiliana na Mkurugenzi ambaye ndiye mwenye timu," alisema meneja huyo.

Mkurugenzi wa Halamashauri ya Geita, Zahara Michuzi alisema wataondoa changamoto zote ambazo waliambiwa ili kukidhi sifa ya kanuni zilizowekwa.

Mbali na Nyankumbu, viwanja vingine ambayo vimepewa agizo ya kufanyiwa marekebisho ni CCM Mkwakwani cha jijini Tanga, Ilulu (Lindi), Ushirika (Kilimanjaro), Mabatini (Pwani), CCM Sokoine (Mbeya) na Jamhuri cha jijini Dodoma.

Michezo
Ijumaa Julai 22, 2022
Nipashe





Fernandes: Ronaldo atabaki Man United

# MANARA NJIA PANDA

●●●Ni baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka miwili kutojihusisha na soka pamoja...

**Na Saada Akida**

UNAWEZA kusema moshi mweusi umezingira katika klabu ya Yanga baada ya msemaji wake maarufu, Haji Manara kufungiwa kujihusisha na soka ndani na nje ya Tanzania kwa muda wa miaka miwili, lakini akitakiwa kulipa faini ya Sh. milioni 20.

Manara alikutwa na hatia katika shauri lililowasilishwa kwenye Kamati ya Maadili ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na sekretarieti ya shirikisho hilo kutokana na vitendo vya ukiukaji wa maadili.

Msemaji huo alidaiwa kumtolea kauli ya vitisho, Rais wa TFF, Wallace Karia katika eneo la VVIP siku ya mechi ya fainali ya Kombe la FA iliyochezwa Julai 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana baada ya hukumu hiyo kutangazwa, Manara alisema hajafanya uamuzi wowote kama atakata rufani au ataitumikia adhabu hiyo kama ilivyotolewa na Kamati ya Maadili.

Hata hivyo, Manara alisema bado hajapokea rasmi nakala ya hukumu ya kamati hiyo inayoongozwa na Mwenyekiti wake, Wakili Mwita Waissaka.

"Sidhani," Manara aliliambia gazeti hili kwa kifupi.

Msemaji huyo wa zamani wa Simba aliendelea kusema anamshukuru Mungu kwa kila jambo.

"Iwe ni jambo la kheri au shari, neno langu kuu ni kumshukuru muumba mbingu na ardhi kwa neno moja kubwa na lenye maana pana sana. Alhamdulillah," Manara alisema.

Rais wa Yanga, Injinia Hersi Said alipotafutwa na gazeti hili jana jioni kuzungumzia hukumu iliyompata Manara, hakupatikana.

Katibu wa Kamati ya Maadili, Walter Lungu alisema kamati hiyo ilijiridhisha na utetezi wa Manara na kumpa hukumu ya kutojihusisha na masuala ya mpira wa miguu pamoja na faini kwa kufuata Kanuni ya Katiba ya TFF kifungu cha 73 (5) na 73 (6).

Lungu alisema kulingana na Katiba na kifungo cha kanuni hiyo ya TFF adhabu hiyo itaanza kutumika rasmi kuanzia jana.

"Baada ya Kamati kujiridhisha kwa ushahidi mlalamikaji na utetezi wa mlalamikiwa, Manara anahukumiwa na matendo hayo baada ya kuitwa mara kadhaa na kukubali kutoa kauli hiyo."

"Julai 11, mwaka huu, kamati ilikutana kwa mara ya kwanza baada ya shauri hilo kuletwa mezani kwetu kwa kuhoji pande zote mbili, kwa upande wa mlalamikaji alileta ushahidi kwa maneno aliyoyasema Manara; "Wewe unanifuatafuata sana, hii ni mara ya tatu, sikuogopi kwa lolote, kwa chochote na huwezi kunifanya chochote, nina uwezo wa kukufanya chochote na huna cha kunifanya," akiwa katika jukwaa la VVIP kwenye mchezo huo," alisema Lungu.

Aliongeza baada ya kuondolewa katika jukwaa kuu alipokwenda kumfanyia taharuki, baada ya mpira kumalizika Manara alimfuata Katibu wa TFF, Wilfred Kidao akiwa na pakti ya boksi ya sigara na kibiriti cha gesi na kurudia maneno hayo hayo.

"Mlalamikiwa alikiri kufanya makosa hayo na aliomba msamaha kwa mlalamikaji lakini kwa wadau wa soka, ila kulingana na kanuni za Katiba ya TFF, Manara atatumikia adhabu hiyo kuanzia sasa," alisema Lungu.

Naye mwenyekiti wa kamati hiyo, Wakili Waissaka alisema Manara anaruhusiwa kukata rufani kama hakuridhika na uamuzi wa kamati yake.

Waissaka alisema kwa hukumu hiyo, Manara hataruhusiwa kushiriki kwa sababu Yanga ni mwanachama wa TFF, hivyo wanatakiwa kufuata maelekezo yasiyoendana kinyume na shirikisho hilo.



Msemaji wa Yanga, Haji Manara ambaye jana alihukumiwa kifungo cha kutojihusisha na masuala ya mpira wa miguu ndani na nje ya nchi kwa muda wa miaka miwili na kulipa faini ya Sh. milioni 20. **PICHA: MAKTABA**

# Simba: Shujaa Sakho

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Simba umesema kitendo cha goli la mshambuliaji wake, Pape Ousmane Sakho kuingia katika fainali ya kuwania Tuzo ya Goli Bora la mwaka la Shirikisho la Soka Afrika (CAF), tayari nyota huyo ameipa heshima kubwa klabu yao.

Jana usiku ndio CAF ilitarajia kutangaza washindi wa tuzo zake katika sherehe maalumu zilizopangwa kufanyika mjini Rabat, Morocco.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema tayari kwake Sakho ni mshindi kabla ya CAF kutangaza matokeo rasmi.

"Leo hii nina furaha kuwa hapa Rabat katika sherehe za tuzo za CAF 2022 pamoja na Pape Sakho. Mungu aendelee kukulinda na kupata tuzo kutokana na juhudi ulizozionyesha. Kwangu wewe tayari ni mshindi. Neno moja kwa shujaa Pape," alisema Barbara.

Goli lililomwingiza Sakho katika tuzo hilo ni lile ambalo alifunga wakati Simba ikicheza dhidi ya Asec Mimosas katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >